**Waziri** aunda timu kuchunguza kusuasua ujenzi kituo cha Mwenge
UKURASA 4



**Chanjo** ya kipindupindu kuanza kutolewa kwa wananchi
UKURASA 17



**Giroud afikisha mechi 100 chini ya Deschamps**
UKURASA 21


# Nipashe

Jumatatu Juni 21, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580618

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# WATEULE WANENA

## • Wadau wafunguka kuhusu uteuzi huo... *Endelea ukurasa 2*



Asia Abdallah



Jerry Muro



Salum Kalli



Colonel Magembe



Gabriel Zacharia

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### WANNE WAHOFIWA KUPOTEA KWENYE HIFADHI YA SERENGETI

WATU wanne wakazi wa kijiji na kata ya Mugeta, Wilaya ya Bunda, mkoani Mara, wanahofiwa kupotelea katika...

UKURASA WA 5

### BASI LILIVYOUA MWALIMU, KUJERUHI WANAFUNZI, WALIMU

MWALIMU Jumanne Mkandilo (30) wa Shule ya Msingi ya Mkombozi Wilaya ya Momba, Mkoa wa Songwe, amefariki...



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (katikati), akimkabidhi cheti Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, cha utambuzi wa udhamini mkuu wakati wa hafla ya uzinduzi wa Umoja wa Wenye Hotel Zanzibar (HAZ). Kulia ni Mwenyekiti wa Umoja huo, Paolo Rosso. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Hofu yaibuka mikorosho ya diwani kufyekwa

UKURASA 4



## Walimu waikataa rasmi Bodi ya Walimu

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA: SASA VUMBI LA POINTI TU UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Mhandisi Rhoben Nkori (kulia), akiteta jambo na Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Mhandisi Consolatha Ngimbwa (katikati) na Naibu Msajili wa Bodi, Mhandisi David Jere, baada ya hafla ya kufungwa kwa mkutano wa nne wa mashauriano na makandarasi wazalendo uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Mwanza. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ma-DC wateule wanena

**Na Salome Kitomari**

WAKUU wa wilaya wateule na wanaomaliza muda wao wa utumishi wamefunguka na kueleza mikakati yao walivyojipanga kuchapa kazi, huku waliachwa wakijivunia alama za maendeleo yaliyogusa maisha ya wananchi kwenye wilaya walizozitumikia.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kwa njia ya simu, wakuu wilaya wapya wateule walimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuwaamini na kuwapa nafasi ya kuwatumikia Watanzania, huku waliomaliza muda wao wakisema kazi waliyoifanya ni sadaka kwa Mungu.

Mkuu wa Wilaya Mteule Wilaya ya Busega, Gabriel Zakaria, alisema uteuzi huo ameupokea kama deni akatimize yale ambayo Rais anataka ayafanye kwa kutumikia wananchi badala ya kusubiri kutumikiwa.

"Hii ni heshima kubwa katika tasnia ya habari...Mungu anipe hekima na kunifundisha namna ya kufanya kazi, nisione mimi nimestahili kuliko wengine, wako wengi lakini kwanini mimi, Mungu anisaidie niweze kulipa deni ya kwamba nimeonekana, nimeaminika na nikatekeleze wajibu wangu," alisema Zakaria ambaye alikuwa Mfanyakazi wa Televisheni ya Taifa (TBC).

Aidha, alisema uandishi wa habari utaendelea kuwapo kwa kuwa ni taaluma yake na ataendelea kufanyakazi hiyo hata baada ya muda wa kuaminiwa na kutumikia kwa nafasi ya DC kwisha,

Mkuu mpya wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Jerry Muro, alijifananisha na askari wa mwavuli ambaye yupo tayari kutumika kokote wakati wowote kwa maendeleo ya wananchi.

"Ninavyoongea na wewe nimesharipoti kazini nipo Ikungi, uteuzi ulinikuta nipo kwenye mkesha wa Mwenge Longido, kazi inaendelea wananchi wa Ikungi wategemee utumishi uliotukuka, hapa ni kama Arumeru kuna majimbo mawili huwezi kwenda bila kupita mjini," alisema.

Alibainisha kuwa anafahamu wilaya hiyo kuna changamoto za migogoro ya ardhi na amepata uzoefu wa kutosha na kuahidi ubunifu katika kutengeneza vyanzo vipya vya mapato, miradi itakayobadilisha maisha ya wananchi, kuongeza kasi ya utoaji wa huduma za jamii, kuitengeneza Ikungi kuwa moja ya wilaya zitazokuwa na uzalishaji wa kutosha wa mafuta ya alizeti kama zao la biashara na kubadili maisha yao.

**ALIYEBAKISHWA**

Naye Mkuu wa Wilaya mteule wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, alisema siri ya kubaki wilayani humo ni kutokana na kufanyakazi kwa ushirikiano mkubwa na wananchi kwa kutatua migogoro na kusimamia shughuli za maendeleo.

"Rais aliahidi kwa wananchi kuwaletea maji, zahanati, kujenga shule na huduma zote za kijamii, usalama wa mali zao na wao wenyewe, sisi wajibu wetu ni kushirikiana kuleta maendeleo na kusimamia rasilimali za taifa kwa kushirikisha wananchi, nimeendelea kuishi kwa kauli ya rais kwa kuishi na shida za watu," alisema.

"Wilaya yangu sehemu kubwa ni vijiji, muda mwingi natumia vijijini nina watu zaidi 400,000 asilimia 80 ni wakulima na wafugaji na asilimia 20 nii wavuvi, Ziwa Victoria lipo wanafanya biashara na kupata kitoweo. Tumetatua migogoro ya ardhi kwa zaidi ya asilimi 100 kwa kwenda kwa wananchi waliko na mara nyingi natatua kwa kushirikisha makundi yote ya jamii," alisema na kuongeza:

"Tulichokifanya ni kuwashirikisha wananchi katika huduma za jamii na wanatuunga mkono juhudi kwa kujitolea nguvu na rasilimali fedha," alisema.

**WALIOTEMWA**

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, alisema anashukuru kwa muda alioaminiwa kwa kuwa utumishi kwake ni sadaka na alisaidia wengi ikiwamo kutatua migogoro ambayo iliibua maadui wengi.

Alisema anaondoka Kilolo akijivunia kusimamia ujenzi wa hospitali ya wilaya, barabara za lami, miradi ya maji mfano Ilulka inayohudumia zaidi ya wananchi 500,000, mradi wa Ruaha Mbuyuni uliokwama kwa muda mrefu na sasa wananchi wanapata maji.

"Kwenye elimu nilikuta wanafanya vibaya ila sasa ufaulu ni asilimia 83 shule ya msingi kutoka 51, sekondari zaidi ya asilimia 90 kidato cha sita kwa asilimia 100 na shule za sekondari kwenye kata nne na vituo vya afya."

"Nimetekeleza majukumu yangu, nashukuru Mungu, namshukuru rais kwa kunipa nafasi, nimefanya ibada kwa wananchi, naacha wilaya imetulia wananchi tulikuwa tunaenda pamoja, wilaya ina utulivu wa hali ya juu, nimeunganisha, nimesimamia sekta zote kwa kadri Mungu alivyonijalia. Ni ibada wakati mwingine unakutana na mtu amekata tamaa unamsaidia na hapo unatengeneza maadui," alisema. Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Ukwerere, Cornel Magembe, alisema alama alizoacha ni kuhamasisha matumizi ya vyoo yalikuwa asilimia 23 na sasa ni 63 , vyumba vya madarasa 400 na kufungua shule mpya na kujenga vyumba vya madarasa, vituo vya afya 20 zahanati 30 kwenye vijiji.

Kuhusu kukatwa alisema: "Rais Nimechukulia maamuzi haya vizuri, Watanzania tuko milioni 60 tunapewa fursa kupima uwezo na kufanya kazi, nilipewa nafasi nikatumika, sasa ni nafasi kwa wenzangu kuingia kutumikia taifa kwa nafasi hizi." Juzi Rais Samia aliuteua wakuu wa wilaya 139 ambao wapo wapya, waliobadilishwa vituo vya kazi na walioondolewa huku waandishi wa habari watano waking'ara kwenye nafasi hizo.


**BANI INVESTMENT LIMITED**
**DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS**

**NOTISI YA SIKU 14/TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA CRDB** tunatoa notisi ya kulipa madeni yenye dhamana tajwa hapo chini ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili.Vinginevyo tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| JINA LA MKOPAJI/MMILIKI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA KUANZIA |
|---|---|---|---|---|
| SHABAN JUMANNE IBRAHIM | Nyumba iliyopo kwenye Kiwanja na.72 | Sengerema Mwanza - | 6.7.2021 | Saa 4:00 asubuhi |
| PETER SABAI CHACHA | Nyumba yenye hati miliki ya kimila na. 34KRG/MKM/0001 | Kisiwani,Hale-Wilaya ya Korogwe Tanga | 6.7.2021 | Saa 4:00 |
| PETER SABAI CHACHA | Shamba na.1285, lenye C.T Na. 23117, L.O Na. 184975. | Kwadoya-Handeni Tanga | 10.7.2021 | asubuhi Saa 4:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba/shamba muda wowote isipokuwa usiku.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224578, 0653134966, 0746 422519**

26317102


# ... Wadau wafunguka uteuzi wa Ma-DC

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wametoa maoni yao kuhusu uteuzi wa wakuu wa wilaya uliofanyika juzi, huku wakipongeza idadi kubwa ya vijana kuaminiwa.

Mhadhiri wa Shule Kuu ya Elimu (DUCE), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam(UDSM), Dk. George Kahangwa, alisema endapo wakuu hao wa wilaya ambao wengi wao ni vijana, watafanya vizuri, Rais Samia Suluhu Hassan atakuwa ametayarisha viongozi wa leo na kesho.

"Ni uteuzi wa vijana ambao majina yao yanajulikana ama kwa kupitia siasa, sanaa au tasnia ya habari, huenda wakawa watu wa kutumia muda mwingi kujifunza na kama wataweza kuchapa kazi na kuongoza kwa hekima, basi mama (Rais Samia) atakuwa ametayarisha viongozi wa leo na kesho," alisema Dk. Kahangwa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Mawasiliano na Uenezi kwa Umma wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Edward Simbeye, alipongeza uteuzi huo kuangalia kwa wingi vijana.

Pia aliwataka vijana walioteuliwa kushika nafasi hizo kwenye wilaya, kuchapa kazi kwa weledi na kuonyesha mfano kwa kuepuka kuwaangusha vijana wengi wenye uwezo walio nyuma yao.

"Hawa vijana walioaminiwa watumie nafasi hiyo kuishauri serikali kuwekeza zaidi kwenye elimu ili kuongeza idadi ya vijana wenye taaluma na kupunguza wasio na taaluma ili kujenga wenye uwezo wa kuajiriwa na kujiajiri, tunaomba wasiende kuharibu huko na kuwaharibia vijana wasiendelee kuaminiwa."

Aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, amesema uteuzi umefanyika kimkakati, huku akidai kuona watu wasio waadilifu wakipewa nafasi, jambo linaloonyesha umuhimu wa Katiba mpya.

"Sina shida na wasanii ambao wao wana vipaji, kuna utofauti kati ya usanii na uhuni, kama kuna wenye mienendo michafu, wahuni halafu wanapewa nafasi ya uongozi unajenga taswira mbaya kwamba uadilifu na tabia njema haistahili kuwa kiongozi," alisema.

"Ma-DC nimewaona kuna vijana wengi, kuna ambao wametulia wana utulivu hawakuwa na mawenge, kuna kundi jipya limeingia ambalo kuna shida kidogo kiasi cha kujiuliza watu wanaomsaidia rais kuteua wanafanyaje kazi ya kuwapata watu hawa, kigezo cha kiuongozi siyo elimu pekee bali na tabia zake kwenye jamii," alisema.

Kwa mujibu wa Lema, Rais hawafahamu watu wote anaowateua bali anasaidiwa na wasaidizi na kwamba kigezo kisiwe vyeti vyao kwa kuwa unaweza kuwa na kontena mbili la vyeti ila kama huna maadili, adabu, na nidhamu wewe sio kiongozi mzuri."

HABARI KITAIFA

# Walimu wakataa uanzishwaji Bodi ya Walimu

**Na Salome Kitomari**

WADAU wa elimu wamekataa uanzishwaji wa Bodi ya Walimu Tanzania na kutaka serikali kupitia upya kuboresha na kuimarisha Tume ya Huduma za Walimu (TSCC), ili kumpunguzia mwalimu mzigo.

Wakizungumza juzi wakati wa kutoa maoni yao kuhusu sheria na kanuni za uanzishwaji wa Bodi ya Walimu ambayo itakuwa na jukumu la kutoa leseni, kunyang'anya leseni, kusajili na kuchukua hatua za kinidhamu kwa masuala ya kitaaluma walimu nchini, walisema badala ya kuanzisha chombo kipya ni muhimu kuimarisha kilichopo.

Wadau hao walitoa maoni yao mbele ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, ambaye aliongoza kama Mwenyekiti wa muda na baadaye kuongozwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Walimu Wakuu Tanzania (TAPSHA), Odas Bambaza, alisema badala ya kuanzisha chombo kipya ni bora kuimarisha TSCC na kuwa na kitengo cha masuala ya kitaaluma ili kupunguza utitiri wa vyombo vya kumhudumia mwalimu na mzigo wa malipo.

"Kuna TAMISEMI, Wizara, TSCC na sasa mnataka tuwe na bodi, wote hao wana mamlaka na mwalimu kwa namna tofauti tofauti hii siyo sawa, ni bora bodi iwe ndani ya TSCC iwape mamlaka ifanye kazi kuliko kuunda bodi ije tena kwa ajili ya mwalimu huyo huyo," alisema.

Naye Mwakilishi wa Chama cha Wamiliki wa Shule Binafsi, Lawrent Gama, alisema ni muhimu TSCC ikaboreshwa kwa kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kuliko kuunda chombo kipya, kilio kikubwa cha walimu ni kwenye ada mbalimbali.

Alitoa mfano ada ya usajili ni Sh. 10,000, ada ya mwaka Sh. 15,000 jumla Sh. 35,000.

"Je, tunaunda bodi kama chanzo cha mapato ili tupate hizi fedha au tunataka kumtetea mwalimu na taaluma, kama tunataka kuboresha basi tubaki na TSCC. Nimeona kwenye kanuni kuna faini za kutosha kwa huyu huyu mwalimu," alisema.

Alisema kukiwa na bodi, mwalimu atapewa leseni ambayo itaonyesha jina la shule aliyopo wakati kwenye sekta binafsi ni kwa mkataba wa mwaka mmoja na mwalimu anaweza kuhama kutoka shule moja kwenda nyingine, na kupendekeza kusiwe na ukomo.

Pia alisema endapo bodi itatoa uamuzi dhidi ya mwalimu fulani atakata rufani kwa waziri, na kwamba kwa kufanya hivyo kutakuwa na tatizo kwa kuwa waziri hatafanyakazi nyingine zaidi ya kupitia rufani za walimu nchi nzima.

Naye Naibu Katibu Mkuu CWT, Maganga Japhet, alisema kanuni zinasema mwalimu asiye na leseni hataruhusiwa kufundisha na ili aajiriwe lazima apitie kwenye bodi jambo ambalo litatengeneza urasimu, na kwamba ni vyema wakaajiriwa na kujiunga na bodi iwe hiari.

"Bodi ni nzuri ila imekuja vibaya, unapewa leseni kwa miaka mitano na baada ya hapo unatakiwa kuhuisha usipofanya hivyo ukakutwa unafundisha unachukuliwa hatua kali ikiwamo faini ya Sh. 500,000, au milioni moja, jela mwaka mmoja au vyote kwa pamoja," alisema na kuongeza:

"Haya hayapo kwenye bodi nyingine za kitaaluma ambazo wengine tupo, hawafuatilii ajira yako. Kulazimisha watumishi wawe kwenye bodi ndiyo waruhusiwe kufundisha hii siyo sawa kabisa," alisema.

Naye mwanachama wa TAPIE, Maxon Binomtonzi, alisema kanuni zimependekeza leseni za aina tatu huku ada, ikiwa ni kila mwaka na kuhuisha kila baada ya miaka mitano jambo alilosema si sawa na ni gharama kwa mwalimu.

Naye Mwalimu Juma Msangi alisema amehitimu chuo kikuu hivi karibuni na kutunukiwa Shahada ya Elimu ya Uchumi na kupewa vyeti ambavyo hukaguliwa mara kwa mara na sasa inakuja bodi.

"Msituone hapa wengine tumesoma kwa shida sana, unategemewa na ukoo baada ya kupata kazi, mshahara huo huo ukatwe makato mengi, tuoneeni huruma kwa vipato vyetu," alisema.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa CWT Temeke, Mohamed Mbonde, alisema hoja kuu ni kwenye gharama za ada, usajili, kupotea kwa leseni ambako kunahitaji fedha kutoka kwa walimu na sababu inayotolewa uanzishwaji wa bodi kuwa kuweka nidhamu ya taaluma ya ualimu wakati wengi wamesoma, lakini hawapandi madaraja.

# Ruzuku yatolewa kuchakata mazao

**Na Mwandishi Wetu, KATAVI**

SHIRIKA la Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA) kwa kushirikiana na Kampuni ya Wataalamu Washauri wa Biashara (TAPBDS), limetoa ruzuku ya ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza mashine za kuchakata mazao mkoani Katavi.

Kupitia mradi wa kusaidia kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno unaoendeshwa na TAPBDS, AGRA imetoa mitambo ya takribani Sh. milioni 100 kwa kiwanda cha kutengeneza mashine cha nondo mkoani humo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mtambo huo, Meneja Mradi kutoka TAPBDS, Joshua Ongaga, alisema lengo la kutoa mitambo hiyo ni kuongeza uzalishaji wa mashine za kuchakata mazao na kurahisisha upatikanaji wake kwa wafanyabiashara na wakulima kwa bei nafuu.

Ongaga alisema awali wafanyabiashara walikuwa wakinunua mashine hizo kwa Sh. milioni 2, lakini kwa sasa mashine hizo zitanunuliwa kwa Sh. 900,000.

Alisema mashine zitakazotengenezwa kupitia mitambo hiyo ni za kusaga mahindi, kukoboa mpunga, kupukuchua maharage, kukamua mafuta ya alizeti pamoja na kuchonga vipuli mbalimbali ili kuongeza thamani ya mazao na kukuza uchumi wa wakulima.

Alifafanua kuwa mbali na mitambo hiyo ya nondo, walitoa mingine minne katika mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya na Rukwa, ambayo yote thamani yake ni zaidi ya Sh. milioni 600.

Mbali na ruzuku ya mitambo kwa wazalishaji wa mashine, mradi huo umewezesha pia wafanyabiashara 31 kutoka mikoa ya Kagera, Kigoma, Ruvuma, Njombe, Iringa, Rukwa na Katavi kwa kuwapa mashine za kuchakata mazao.

Mkurugenzi na Mmiliki wa Nondo Investment, Raymond Kamtoni, alisema kampuni inakusanya mazao kutoka kwa mtandao wa wakulima, vyama vya ushirika na wakulima wenyewe.

Alisema wameajiri wataalamu wa kilimo sita kwa ajili ya kutoa elimu kwa wakulima ya kulima kilimo chenye tija na kitakocholeta manufaa kwao.

Kuhusu kiwanda, alisema kina uwezo wa kusaga mahindi tani 25, mpunga tani 20 na mafuta ya alizeti tani tano hadi 10 kwa mwezi na wana mpango wa kufunga mashine nyingine ya kuchuja hadi tani 20. Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwamvua Mrindoko, akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi huo, alisema mkoa wake unategemea kilimo kwa asilimia 90 hivyo kupitia mradi huo unaenda kukuza uchumi wake kwa kasi.






Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo za Vikoba, Dk. Amina Abdul (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam wakati wa kutangaza maandalizi ya tuzo hiyo kwa vikundi mbalimbali vya kuweka na kukopa nchi nzima zinazoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Women Supporting Women, zitakazofanyika mwishoni mwa mwezi Agosti 2021. Kulia ni Yasinta Bokela Mwanachama Mwasisi wa Tuzo hizo, Meneja Mauzo wa BankABC, Bertha Bash (wapili kulia) pamoja na Meneja Masoko wa BankABC, Rose Ngowi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hofu yaibuka kijijini Mtwara mikorosho ya diwani kufyekwa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WATU ambao hawajafahamika, wameingia katika shamba la diwani mstaafu wa Kata ya Namangwa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, Edwin Kasembe na kukata zaidi ya mikorosho 50.

Shamba hilo lipo katika Kijiji cha Mkoropola, huku ikielezwa kwamba tukio hilo lilitokea usiku wa manane huku ikidaiwa wahusika walitumia vitu vyenye ncha kali kama mapanga.

Wakizungumza na gazeti hili jana kijijini hapo, baadhi ya wananchi walisema kuwa wameingiwa hofu ya usalama wa mikorosho yao kwa sababu huenda ni kikundi ambacho kimejipanga kuharibu mikorosho ya wakulima.

Salumu Bakari, alisema kitendo hicho cha watu hao kukata mikorosho kinatafsiriwa kama ni jambo la kisiasa.

Alisema wananchi wengi wakijiuliza maswali ya kutaka kufahamu ni kwa sababu gani watu hao wameamua kufanya hivyo.

Naye Fatuma Issa alisema wananchi hivi sasa wanatumia muda mwingi kupita katika mashamba yao kuangalia kama mikorosho bado ipo.

"Hatujapendezwa na hili tukio, kwa sababu ni la kinyama sana, kukata mikorosho zaidi ya 50 ni kuharibu uchumi wa mtu... hatuwajui hawa watu walikuwa na malengo gani, maana tukio kama hili halijawahi kutokea hata mara moja hapa kijijini," alisema Issa.

Diwani huyo mstaafu Kasembe alisema alisikitishwa na kitendo hicho, na kwamba baada ya kupata taarifa kutoka kwa wakazi wa kijiji hicho kuhusu uharibifu huo.

Kasembe alisema shamba lake lina zaidi ya mikorosho 300, na mikorosho ambayo imekatwa na watu hao ni zaidi ya 50 ambayo ilishaanza kutoa korosho, hivyo tukio hilo limemsababishia hasara kubwa kwa kuwa shamba lake amelihudumia kwa gharama kubwa.

"Nimeshtushwa sana baada ya kupata taarifa hizi za kukatwa mikorosho yangu lakini nimeshachukua hatua ya kutoa taarifa kuanzia ngazi ya serikali ya kijiji pamoja na kituo cha polisi cha Wilaya ya Masasi," alisema Kasembe.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mkoropola, Tadeus Nyang'ama, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa uongozi wa serikali ya kijiji ulishafika katika shamba hilo na kujionea hali halisi na kwamba jambo hilo limezua taharuki kwa wananchi hasa na wao kuhofia watu hao kuingia katika mashamba yao kukata mikorosho yao.

Alisema serikali ya kijiji ilishaitisha mkutano wa kijiji na kueleza jambo hilo na kwamba uamuzi uliofikiwa ni kufanya uchunguzi dhidi ya wahusika wa tukio hilo ili sheria ichukuwe mkondo wake.


**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY**
**AT DAR ES SALAAM**

**CIVIL APPEAL NO. 346 OF 2020**

**(From the judgment of Civil Appeal No. 28 of 2018 before Hon. Ebrahim, J delivered on 26/6/2020, Originating from Kinondoni District Court in Civil Case)**

**DOREEN PONDAMALI.........................................APPLICANT**
**VERSUS**
**LATIFA MULIKA....................................RESPONDENT**

**SUMMONS FOR PUBLICATION**

**TO: LATIFA MULIKA, DAR ES SALAAM.**

**WHEREAS,** the above mentioned case has been fixed for mention **29TH day of July, 2021 at 9:00 AM** before **Hon. DR. J. L. MASABO – Judge** you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence.

**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of Court this **9th day of June, 2021.**

THE HIGH COURT OF TANZANIA

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM


# Mradi ujenzi kituo cha Mwenge kuchunguzwa

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameagiza kuundwa kwa timu ya uchunguzi kwenye Mradi wa Kituo kipya cha Daladala Mwenge, jijini Dar es Salaam, baada ya ujenzi wake kusuasua.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea ujenzi wa kituo hicho, Waziri Ummy alisema hajaridhishwa na kasi ujenzi wa kituo hicho na anapokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi.

"Huu mradi ulipaswa kukamilika Mei 2, mwaka huu, lakini hadi sasa ni Juni na ujenzi wake umefikia asilimia 46, nasimamisha ujenzi wake kuanzia sasa na kuunda timu ya kuchunguza," alisema Waziri Ummy.

Alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI kuunda timu hiyo haraka na kueleza kuwa itafanya kazi katika kipindi cha wiki mbili, kuachunguza pia miradi miwili ambayo ni ujenzi wa uwanja wa mpira wa Manispaa ya Kinondoni, ujenzi wa jengo la Utawala la Manispaa ya Kinondoni.

Pia alitangaza kumsimamisha kazi Mhandisi wa Manispaa ya Kinondoni, Isaak Mpaki, kutokana na kushindwa kuishauri vizuri Manispaa ya Kinondoni ujenzi wa miradi hiyo mitatu.

"Kuna figisu kwenye hii miradi, miradi haikamiliki, kila mtu anasema la kwake, huu mradi (stendi ya Mwenge) ungekamilika ungeingiza faida ya Sh. milioni 480 kwa mwaka, tungejenga shule, hospitali, lakini hadi sasa hakuna kitu," alisema Waziri Ummy.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Spora Liana, alisema gharama ya ujenzi wa mradi huo ni Sh. bilioni 4.898, na mkandarasi (361 JWT Lugalo) alikabidhiwa mradi Julai 27, mwaka jana.

Alisema ilipofika Mei 2, mwaka huu, ujenzi wa mradi huo ulifikia asilimia 46, hadi sasa Sh. bilioni 1.558 zimeshatumika.

"Changamoto kubwa ni vifaa kutoagizwa kwa wakati, vibarua wachache ambapo mkandarasi badala ya kutumia askari anaajiri raia, pamoja na kuchelewa kulipwa mishahara yao na kuja ofisi kwangu kunilalamikia," alisema Liana.

Mkandarasi wa mradi huo, Luteni Kanali David Luoga, alisema Aprili mwaka jana walianza kazi ya ujenzi wa stendi hiyo, kazi yao ni kujenga, lakini vifaa vya ujenzi vinaletwa na Manispaa ya Kinondoni.

"Ilipofika Julai mwaka jana, mtiririko wa vifaa haukuwa mzuri, vikawa vinakuja kwa kusuasua, ilipofika Septemba tuliandika barua ya kuomba vifaa vyote vinavyohitaji kufika eneo la mradi, lakini hadi sasa havijafika," alisema Luteni Kanali Luoga.

Alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo ni kutokuwapo kwa utekelezaji wa maamuzi yaliyoingiwa, viongozi wa Manispaa ya Kinondoni kutokuwa na maamuzi.

# Wanne wahofiwa kupotea hifadhini

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

WATU wanne wakazi wa kijiji na kata ya Mugeta, Wilaya ya Bunda, mkoani Mara, wanahofiwa kupotelea katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, wanakodaiwa kwenda kufanya uwindaji haramu. Viongozi wa wilaya hiyo akiwamo Mwenyekiti wa Kijiji cha Mugeta, Manekela Gashaka na Diwani wa kata hiyo, Mganga Jongora, juzi wakizungumza na gazeti hili walithibitisha kuwapo kwa tukio hilo.

Walisema kuwa watu hao wakiwa idadi ya watano wanadaiwa kwenda katika hifadhi hiyo Mei 29, mwaka huu, saa za mchana. Waliwataja watu hao kuwa ni Shakanyi Marinta (29), Nyachuma Nyachuma (49), Mashaka Petro (35) na Giromora Kahema (31), wote wakazi wa Kijiji cha Mugeta, wilayani Bunda.

Walisema taarifa waliyopata kutoka kwa mmoja wa wawindaji hao Kwakwa ya Kibina (29), aliyebahatika kukimbia na kwenda kutoa taarifa kijijini, ni kwamba siku ya tukio wakiwa hifadhini walikurupushwa na askari wa hifadhi hiyo na kukimbia huku wengine wanne hawajapatikana na hawajulikani walipo.

"Ni kweli kuna vijana watano waliokuwa wameenda huko hifadhini Serengeti, mmoja wao alikimbia hadi kijijini, lakini wale wanne hadi leo hii bado hawajulikani walipo," alisema Diwani Jongora.

"Walikuwa watano huyo mwingine alituambia kwamba, wakiwa katika eneo hilo walikurupushwa na askari na ndipo walipokimbia na mmoja akafika hadi kijijini na kutoa taarifa hiyo," alisema Mwenyekiti wa kijiji hicho, Gasheka.

Mmoja wa wana familia, Anna Marinta, ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Mugeta, alisema kuwa baada ya kupata taarifa hiyo Mei 29, mwaka huu, walianza kufuatilia kwenye vituo vya polisi na magereza ya mikoa ya Mara na Simiyu, lakini hawakuwapata ndugu zao, hali iliyowafanya kuwa na wasiwasi.

"Tulifuatilia kwenye vituo vya polisi, maana tunajua kwamba wakikamatwa lazima wapelekwe polisi, lakini hatukuwapata. Pia tukaenda kuwatafuta kwenye magereza mbalimbali hadi kwenye ya mkoa wa Simiyu, lakini bado hatujawaona. Sasa tumeona tuwatumie nyie watu wa vyombo vya habari mtusaidie," alisema Anna.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Massana Mwisawe, akizungumza kwa njia ya simu na gazeti hili jana, alisema hajapata taarifa yoyote ya kuwapo kwa tukio hilo.

Aidha, alipotafutwa kwa njia ya simu, Ofisa Uhusiano wa SENAPA, Robert Masobheji, simu yake iliita bila kupokelewa na alipotafutwa tena simu ilikuwa haipatikani. Marinta, alisema wameshawatafuta ndugu zao tangu siku walipopata taarifa Mei 29, bila mafanikio na sasa wanaomba msaada wa serikali, ili kujua mahali walipo ndugu zao.

> **"Ni kweli kuna vijana watano waliokuwa wameenda huko hifadhini Serengeti, mmoja wao alikimbia hadi kijijini, lakini wale wanne hadi leo hii bado hawajulikani walipo,"**

# Wadau wataka uwekezaji elimu ya umeme

**Na Faustine Feliciane**

WADAU wa umeme nchini wamesema ni muda sahihi kuwekeza kwenye elimu ya umeme kipindi hiki ambacho serikali inaendelea na mikakati ya kuwekeza na kusambaza nishati hiyo mijini na vijijini.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya 'Elimu Umeme Foundation', Mkurugenzi Mkuu wa Geared Consulting Engineeers Ltd, Mhandisi Warda Ester Mash'mark, alisema mfumo wa umeme kama ilivyo mifumo mingine inafuata viwango vya kitaifa na kimataifa ambavyo hubadilika.

"Lengo kuu la taasisi hii ni kufundisha jamii matumizi sahihi na salama ya umeme ikiwamo miundombinu yake na pia kushirikiana na serikali kuboresha mitaala shuleni, taasisi za ufundi na vyuoni.

Kupitia Elimu Umeme Foundation tutashiriki kikamilifu kutoa elimu inayohusu masuala ya umeme," alisema.

Alifafanua kwa kutoa mfano tangu mwaka 2004 rangi za nyaya za umeme zilifanyiwa mabadiliko, ambayo yalisababisha kubadilishwa ngazi ya kitaifa (TBS-2012). Hata hivyo, alisema kuna mkanganyiko kwa sababu kuna rangi za zamani ambazo bado ziko sokoni.

Vilevile, alisema kwa upande wa matumizi ya umeme wateja kama viwandani, majengo na wengine wengi kutokana na kukosa elimu ya viwango vya umeme, wanalipa gharama kubwa na bidhaa zinazozalishwa nchini hukosa ushindani sokoni kutokana na gharama ya uzalishaji.

"Hii imekuwa ikisababisha wadau wengi zikiwamo taasisi za serikali na binafsi wakati mwingine kushindwa kulipa ankara na kusababisha kukatiwa umeme, hii yote inatokana na ukosefu wa elimu na hivyo sisi tumeamua kuja na Elimu Umeme Foundation kusaidia kutoa elimu," alisema.

Alisisitiza kwamba serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imewekeza kwenye uzalishaji na usambazaji umeme na kasi hiyo iandane na wananchi kuujua umeme na kuchukua tahadhari zote ili kuepuka majanga yakiwamo vifo.

"Tunaiomba serikali na taasisi binafsi zituunge mkono kwa hali na mali ili uwekezaji kwenye umeme uende sambamba na elimu," alisema Mhandisi Mash'mark.

Alisisitiza kazi ya kutoa elimu ni ngumu kutokana na matatizo kwenye mifumo ya umeme kuwa mengi, lakini wameanza kutekeleza kinachokwamisha ni gharama za uendeshaji na ushirikiano duni kutoka taasisi za kiserikali.

Kwa upande wake Kamanda wa Jeshi la Zimamoto Kinondoni, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Isack Njombe, alisema taasisi hiyo kwa namna moja au nyingine wanalisaidia Jeshi la Zimamoto katika kutoa elimu ya matumizi sahihi ya umeme.

Alifafanua kuwa majanga mengi ya moto yanatokana na hitilafu za umeme ambazo nyingine zinatokana na kukosekana kwa elimu sahihi ya matumizi ya nishati hiyo.

# Basi lilivyoua mwalimu, kujeruhi wanafunzi, walimu

**Na Mwandishi Wetu,** SONGEA

MWALIMU Jumanne Mkandilo (30) wa Shule ya Msingi Mkombozi Wilaya ya Momba Mkoa wa Songwe, amefariki dunia katika ajali ya barabarani.

Alikutwa na mauti kufuatia ajali ya gari lililokuwa limebeba wanafunzi waliokuwa wakitokea mkoa wa Mtwara kwenye michezo ya kitaifa ya UMITASHUMTA, huku 11 wakijeruhiwa wakiwamo wanafunzi saba, walimu watatu na kondakta.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi usiku katika kona za Kijiji cha Kilimasela kilichoko Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma.

Kamanda Maigwa alilitaja basi lililokuwa limewabeba abiria 42, huku wanafunzi wakiwa 35, walimu na wafanyakazi wa gari hilo aina ya Mitishubishi Fuso mali ya kampuni ya Mega, lilimshinda dereva kwenye kona za Kilimasela kisha kupoteza njia na kupinduka, hivyo lililosababisha kifo cha mwalimu Jumanne Mkandilo.

Alisema majeruhi walipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Ruvuma.

Maigwa alisema katika uchunguzi wa awali inadaiwa dereva huyo alikuwa kwenye mwendokasi, hivyo kushindwa kuimudu kona hiyo.

Mwanafunzi Datin Mbuya wa Shule ya Msingi ya Mlangali Wilaya ya Mbozi, alisema walipofika kwenye kona za Kilimasela wakati wa usiku huku baadhi ya wanafunzi wengine walikuwa wamesinzia na kuwa alishangaa gafla gari linaingia kwenye korongo ambalo alidai kuwa ni refu na hapo kila mmoja alikuwa analalamika kumwomba Mungu awanusuru.


NEW OFFICIAL DEUTZ PARTS AND SERVICE DEALER IS NOW OPEN IN TANZANIA

As the official service dealer and partner of Deutz Corporation, Mantrac Tanzania offer complete service and maintenance on Deutz diesel engines.
We handle everything from preventive maintenance to overhauls – all with the intention to increase the lifetime of your engine.

YOUR ONE SAFE SOURCE

Mantrac is one of the world's leading authorised Caterpillar dealer representatives, meaning we're an expert in the industry of supplying the best in market solutions for a range of applications and industries.



Mantrac Tanzania
Plot no 4A, Nyerere Road
P.O. Box 9262
Dar es Salaam

DEUTZ GENUINE PARTS COME WITH UP TO 12-MONTHS WARRANTY*

*Terms & conditions apply

0689 552 011
www.mantrac.co.tz

MANTRAC AFTERMARKET
DEUTZ
26284002

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Wachezaji msiamue usajili kwa kumulika pesa pekee*

**VUGUVUGU** la kuelekea dirisha la usajili tayari limepamba moto licha ya kwamba dirisha hilo halijafunguliwa kutokana na msimu wa 2020/21 kubakisha takriban raundi nne kabla ya kumalizika kwa timu ambazo hazina viporo.

Tayari baadhi ya klabu zimeshaanza kuingia mikataba ya awali na wachezaji walionyesha kiwango cha kuvutia msimu huu, lakini ikiwa ni kwa wale ambao mikataba yao inatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu.

Kwa ujumla ni uamuzi mzuri kwani hadi kufikia hatua hii, kila timu imeshajua udhaifu wake na maeneo inayopaswa kuyaimarisha ili kuingia msimu mpya wa 2021/22 ikiwa imara kuweza kutoa ushindani mkubwa kwenye ligi hiyo itakayojumuisha timu 16 kutoka 18 za msimu huu.

Hata hivyo, kila msimu tumekuwa tukishuhudia klabu kubwa nchini hususan Simba, Yanga na Azam FC, zikisajili wachezaji hadi watatu katika nafasi moja, na kuishia kwenda kusugua benchi hadi msimu unamalizika na kisha kuachwa msimu unaofuata.

Tunachokiona katika hilo, ni wachezaji wengi kutazama zaidi kiasi kikubwa cha fedha wanachopewa kwa ajili ya kusaini mkataba, lakini mshahara mkubwa wanaokwenda kulipwa kwa kusugua benchi hadi klabu wazozichezea kwa sasa ama wanazotoka.

Hivyo, kuelekea dirisha jipya la usajili, Nipashe tunawakumbusha wachezaji kutoishia kuangalia kiasi cha pesa wanazopewa kwa ajili ya kutia saini mkataba ama mishahara mikubwa wanayokwenda kuipata, bali hayo yote yanapaswa kuambatana na kupata nafasi ya kucheza.

Tunatambua nafasi ya kucheza haiwezi kuja pasipo kwenda kuonyesha jitihada kuanzia mazoezini hadi wanapopata nafasi katika mechi, hivyo wanachopaswa kukitazama si kuogopa ama kukataa kusajiliwa bali kila anayetakiwa na klabu hizo hana budi kujipima kwanza na akiona anatosha kwenda kupambana ndipo asaini mkataba.

Ni wazi wachezaji wengi wa ndani/wazawa wanaosajiliwa na klabu hizo kubwa, wamekuwa wakishindwa kutoa ushindani wa namba kutoka kwa nyota wa kigeni wa klabu hizo, matokeo yake wanaishia kusugua benchi na baadaye kuachwa.

Katika hilo, si kwamba tunawakatisha tamaa kujiunga na klabu hizo, bali cha muhimu ni kila mmoja kujitambua kwa nafasi yake na kutoishia kuridhika na mshahara mkubwa wakati hachezi.


Tunaamini kwa mchezaji ambaye ana malengo ya kufika mbali zaidi ya Simba, Yanga na Azam, anaweza kusajiliwa na timu hizo na kwenda kupambania namba na nyota wa kigeni wa klabu hizo na hatimaye ndoto zake kutimia, lakini si kwa wale wanaomulika maslahi pekee.

Lakini, kwa wachezaji ambao wanajipima na kuona hawatoshi kwenda kuwaweka nyota wa kigeni benchi katika timu hizo, huu si wakati muafaka kwao wakukubali kubweteka na kiasi kikubwa cha mshahara ambacho kitamfanya kuporomoka kiwango na kupotea kabisa.

Tunachotaka kukiona ni wachezaji wazawa kuzidi kupata nafasi na kuwa msaada kwa timu zetu za taifa, lakini hilo haliwezi kutokea kama kila mmoja hatoonyesha moyo wa kupambana na nyota wa kigeni waliowazidi uwezo.

Lakini, kuliko kukimbilia kusajiliwa na timu kubwa kwa kutazama fedha pekee, ni bora kubaki katika klabu zao sehemu ambazo watapata nafasi ya kucheza mara kwa mara jambo ambalo si tu litasaidia kuboresha viwango vyao na kuwaimarisha, bali watakuwa msaada kwa timu zetu za taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Lengo la vijana U-20 ni vipaji si kutwaa mataji*

Na Adam Fungamwango

**DAKIKA** chache kabla ya mechi ya fainali ya vijana chini ya miaka 20 kati ya Yanga na Mtibwa Sugar kumalizika, kulitokea vurumai baada ya mshika kibendera kukataa bao ambalo lingekuwa la kusawazisha kwa yosso hao wa Jangwani.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Azam Complex, Mtibwa Sugar ilitwaa ubingwa wa michuano hiyo kwa mara ya tatu mfululizo kwa kushinda mabao 2-1.

Baadhi ya mashabiki wa Yanga walimtupia chupa za maji mwamuzi wa pembeni aliyekataa bao.

Wakati mchezaji Abdulkarim Yunus anafunga bao, mchezaji mmoja wa timu hiyo, Yohana Ndushi aliingilia mchezo.

Mpira ulisimama kwa muda, lakini baadaye ukaendelea na mabao 2-1 yaliendelea kuwa hayo hayo hadi mwisho wa mchezo.

Kwanza kabisa niipongeze timu ya vijana wa Mtibwa Sugar ambayo imetwaa ubingwa huo mara ya tatu mfululizo.

Hii inaonekana kuwa haibahatishi. Ni kwamba viongozi wa Mtibwa Sugar wanajipanga na kuleta timu halisi ya vijana iliyokaa kambini kwa muda mrefu.

Ukiangalia timu hiyo na wachezaji wote, utaona kabisa kuwa lengo la viongozi wa Mtibwa ni kusaka wachezaji wenye vipaji vya soka na kuwaweka pamoja. Lengo likiwa ni baadaye kuwapandisha kwenye kikosi cha kwanza, ili kufanya biashara ya kuwauza kwa timu yoyote inayohitaji.

**Ukiangalia timu hiyo na wachezaji wote, utaona kabisa kuwa lengo la viongozi wa Mtibwa ni kusaka wachezaji wenye vipaji vya soka na kuwaweka pamoja.**

Hapo kuna faida mbili. Kupata wachezaji wa kucheza Ligi Kuu bila kutumia gharama kubwa za usajili, pia kuuza na kupata pesa za kuendeshea klabu. Inawezekana kabisa kuwa Mtibwa Sugar inapata wachezaji wazuri kirahisi kutokana na kuwa ipo kwenye mkoa ambao miaka nenda rudi inatoa vipaji vya wacheza soka nchini, lakini inaonekana pia viongozi wa Mtibwa Sugar wako makini kusaka vipaji na si kukusanya wachezaji vijana kwa ajili ya michuano fulani.

Ndiyo maana utaona wachezaji karibuni wote wa Mtibwa, kila mmoja ana kipaji chake tofauti, huku muunganiko wa wachezaji ukiwafanya kuwa timu tishio kwa zingine. Na inaweza kuendelea hivyo miaka mingine inayokuja kama viongozi wa timu zingine hawatojirekebisha. Angalau Azam FC unaweza kusema ina vijana wazuri, lakini bado wengi wanahitaji mafunzo zaidi na kukaa kwa muda mrefu.

Ukiangalia timu za vijana kama za Simba na Yanga unaona zina baadhi timu ya wachezaji wawili watatu ambao wana vipaji halisi vya soka. Wengi ni wa kawaida tu ambao unaweza kuwapata kwenye timu yoyote ile. Hapo unaanza kujiuliza, huwa wanakusanywa wakati wa michuano kama hiyo tu? Au kwa sababu klabu kubwa, basi kuna wazazi hulazimisha kuwapeleka watoto wao kwa kuwatumia watu wanaojuana nao?

Nilitegemea timu za Simba na Yanga zingekuwa na watu wa kusaka vipaji kila kona ya nchi na kuwa na kikosi cha kutisha mara tatu au nne ya kile cha Mtibwa Sugar.

Na lengo la kusaka wachezaji hao ni kupata wachezaji wazuri wa Kitanzania ambao baadaye watazitumikia timu za wakubwa na timu ya Taifa, Taifa Stars, ili kuokoa pesa nyingi kwenye usajili.

Badala yake inaonekana kuna baadhi ya timu zilikusanya wachezaji kwa ajili ya kutafuta ubingwa tu wa Ligi ya Vijana. Ndiyo maana unaona hata baadhi ya mashabiki wa Yanga walianza kufanya vurugu baada goli la kukataliwa.

Mashabiki wengi wanashindwa kujua kuwa lengo la timu za vijana si kuchukua mataji, ila ni kuwa na vijana bora watakaokuwa hapo kwa faida ya kuchezea timu kubwa baadaye, na si baada ya michuano timu inavunjwa na kuundwa tena ikikaribia tena michuano.

Timu inaweza kutwaa ubingwa, lakini isiwe na wachezaji bora, lakini ikaishia njiani ikawa na wachezaji wenye vipaji. Vipaji na uwezo ndiyo unaotakiwa kwenye michuano hiyo, na si ubingwa, ingawa Mtibwa Sugar wametisha kwa vipaji na kuchukua pia ubingwa. Hongera nyingi ziwafikie.

# TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MARUDIO:
## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA YA KUJENGA NYUMBA MBADALA KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP)
## KUMBUKUMBU NA: 0010006840

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalika makampuni yenye uzoefu na sifa kutuma nia ya kujenga nyumba mbadala kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha Mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta hayo katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni karibia kilomita 1,443, kati hizo kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania. Katika upande wa Tanzania bomba litapita katika mikoa nane (8), halmashauri za wilaya 27 na vijiji 231.

### MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

Ujenzi wa nyumba mbadala na majengo tegemezi (jiko na vyoo) kwa Waguswa wa Mradi (PAPs) wanaohamishwa na Mradi wa Bomba utafanyika katika mikoa nane tofauti; Kagera, Tabora, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Manyara na Dodoma.

Mradi utajenga nyumba mbadala katika ardhi iliyokubalika kwa waguswa stahiki wanaohamishwa makazi. Mradi utabainisha aina za muundo wa majengo mbadala yatakayojengwana maeneo kwa makubaliano na kila Mguswa wa Mradi. Mkadarasi atajenga nyumba 336, Vyoo vilivyoboreshwa vyenye mfumo wa kuzungusha hewa 388 na majiko ya nje 345 kutokana na michoro iliyosanifiwa kwa kina na Kampuni ambayo yote imeandaliwa kwa viwango vya usawa vya ujenzi wa nyumba.

Muundo wa chini na juu (msingi uliofungwa nondo na kumwagiwa zege, kuta za ndani/nje) kwa kila nyumba pamoja na nyumba tegemezi zitajengwa kwa kutumia vifaa vya vipimo vitakavyotolewa na Kampuni na vinavyoweza kutumika zaidi ya mara moja na kwa kutumia mseto wa zege uliosanifiwa kwa kazi husika.

Wakandarasi wote watategemewa kufanya kazi kwa kutumia mfumo huu wa vifaa vya vipimo vitakavyotolewa. Ukamilishaji wa kazi yote inayobakia (vibarua na rasilimali) kama vile kupaua, kukamilisha ujenzi, umeme na miundo mbinu ya maji safi na maji taka, kazi za ujenzi na uboreshaji wa muonekano wa ardhi zitakuwa ni jukumu la Mkandarasi.

Wazabuni watakao kidhi vigezo vya awali watapokea taarifa za muundo wa vifaa vyenye vipimo vitakavyoonyesha wazi na kuwa na taarifa za kina juu ya utengenezaji wa bidhaa husika.

Nyumba mbadala kwa ujumla zitakuwa zina kati ya vyumba viwili mpaka vitano, vyenye ukubwa wa eneo la sakafu wa mita za mraba 25 mpaka 75. Kila nyumba itakuwa na miundombinu tegemezi miwili, yaani jiko na choo cha shimo kilichoboreshwa chenye mfumo wa kuzungusha hewa. Nyumba mbadala zitakuwa za kiwango bora cha ujenzi. Kwa muundo wa chini na juu wa nyumba, nyumba zote zitajengwa kwa kutumia malighafi zinazopatikana katika maeneo husika, zote zitakidhi viwango vya ujenzi vya ubora vya Tanzania .

### VIGEZO MUHIMU:

Kutokana na ukubwa wa kazi na ili kuyasaidia makampuni yanayoonyesha nia, Mradi una haki ya kutoa kazi moja moja au pia kazi zaidi ya moja kwa mkandarasi atakayeonyesha nia na mwenye kukidhi vigezo. Kampuni zenye nia zinaweza kuingia mikataba na kampuni nyingine ili kuwezesha uwezo wao wa kutoa huduma, lakini wote kwa Pamoja na kila mbia katika mkataba ni LAZIMA akidhi matakwa tajwa yaliyoainishwa hapo chini.

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Kampuni ya Kitanzania ya Ukandarasi (Ujenzi) iliyosajiliwa kwa kiwango cha chini cha daraja la pili (wasilisha nakala),
- Mifano ya uzoefu wa kujenga majengo katika mkoa wa Kagera, Tabora, Geita, Shinyanga, Singida, Manyara na Dodoma Tanzania. (Wasilisha orodha ya miradi iliyofanyika katika mkoa wowote tajwa au mikoa yote),
- Thibitisha uwezo wa kifedha wa kutekeleza kazi tajwa,
- Thibitisha/wasilisha sera za Afya, Usalama na Mazingira (HSE/OSHA), na Usimamizi wa Viwango vya Ubora na maswala ya Jamii,
- Wasilisha/Thibitisha uzoefu wa kusimamia miradi, utaratibu wa ugavi na usafirishaji vitu Pamoja na manunuzi,
- Dhamira ya kuongeza thamani katika uwezo wa ndani/taifa (wasilisha taarifa za kina za mafunzo),
- **Uthibitisho wa usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) ya EWURA wakati wa kuwasilisha taarifa ya nia unahitajika.**

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: tolal.mufti@external.total.com (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **15 Julai 2021.**

Taarifa ya kina itawasilishwa na Kampuni ili kutoa taarifa zaidi kuhusu huduma, ratiba ya utekelezaji pamoja na kutoa kipindi cha maswali na majibu kutoka kwa wazabuni wenye nia - undani wa taarifa utawasilishwa katika hatua ifuatayo.

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya Makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

# Mbunge: Bajeti ya kisayansi inayopanua wigo wa kodi

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Munde Tambwe, amesema bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22 ni ya kisayansi inayokwenda kupanua wigo wa kodi ambayo haitamuumiza mwananchi.

Akichanga bajeti hiyo mwishoni mwa wiki bungeni jijini Dodoma, mbunge huyo alihamasisha Watanzania kuipokea ili ikalete mabadiliko ya nchi yao.

"Dunia nzima hakuna nchi isiyolipa kodi ila inategemea ni kodi za aina gani ambazo wananchi watazimudu, mfano kodi ya majengo nimesikia kuna watu wanaiongelea wakisema italeta mkanganyiko baina ya mwenye nyumba na mpangaji," alisema na kuongeza;

"Nchi hii ina wataalamu na nyumba zetu zina hati kwa hiyo wataangalia nyumba hii hati ni ya nani, niwatoe wasiwasi Watanzania wanaosema huu ni mkanganyiko."

Munde alisema ikitokea kwa bahati mbaya mpangaji akakatwa kodi ya jengo stakabadhi itaandikwa ili siku atakapoanza mkataba mpya na mwenye nyumba wataiweka mezani ili ikatwe kwenye mkataba.

Aliwataka Watanzania kuzipokea kodi hizo kwa sababu hazilengi kuwaumiza badala yake serikali itaongeza mapato na kutekeleza shughuli za maendeleo. "Tunahitaji Sh. trilioni 36 ili kutekeleza shughuli za maendeleo ni lazima Watanzania tulipe kodi hatuwezi kuwa na nchi ambayo wananchi wake hawalipi kodi tumuunge mkono Rais Samia Suluhu Hassan, kuhusu suala la kodi ya simu siyo kweli mtu akiamka asubuhi anakatwa bali akiweka muda wa maongezi watakatwa kuanzia Sh. 10 na kuendelea," alisema.

Alisema ukusanyaji wa kodi wa aina hiyo utaiwezesha Tanzania kupiga hatua kimaendeleo. Kuhusu bodaboda Munde alisema kundi hilo kwa muda mrefu lilikuwa linaumia na kodi kubwa ya Sh. 30,000 na kwamba serikali imewapunguzia mzigo mkubwa.

"Suala la madiwani kulipwa posho moja kwa moja na serikali ni jambo zuri kwa sababu watapata fedha zao kwa wakati muafaka kwa sababu madiwani wangu wana miezi sita hawajalipwa," alisema.

Kadhalika, alisema tangu uhuru haijawahi kutokea awamu ikalipa posho ya madaraka kwa Mtendaji Kata na Katibu Tarafa na kuomba suala hilo liungwe mkono.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akionyesha kifaa cha UMETA kwa wanakijiji wa Namtumbuka, Kata ya Namtumbuka, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba, Wilaya ya Mtwara, mkoani Mtwara ambapo uzinduzi wa mradi kabambe wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa pili katika mkoa wa Mtwara, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matatani madai ya bangi, wizi wa simu

**Na Gurian Adolf,**
SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linawashikilia watuhumiwa watano (majina yamehifadhiwa) kwa makosa tofauti likiwamo la mmoja kati yao kukamatwa akiwa na kete 584 za dawa za kulevya aina ya bangi.

Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, William Mwampaghale, alisema kukamatwa kwa watuhumiwa hao kumetokana na operesheni maalum inayofanywa na jeshi hilo kwa lengo la kumaliza vitendo vya uhalifu mkoani humo.

Katika tukio la kwanza, polisi walimkata mtuhumiwa akiwa na kete 584 za bangi amezibeba kwenye begi ndogo mkononi kwa lengo la kuipeleka kuiuza.

Alisema kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo kulifanikiwa baada ya polisi kupata taarifa za siri kutoka kwa raia wema.

Katika tukio la pili, alisema watu wanne walikamatwa, mmoja anashikiliwa akiwa na simu ambayo inadhaniwa ni mali ya wizi aina ya Tecno K7 yenye IMEI 354387096412708/16 rangi nyeusi yenye thamani ya shilingi 270,000.

Kamanda Mwampaghale alisema mtuhumiwa mwingine alikamatwa akiwa na simu aina ya Samsung Gallax yenye IMEI yenye thamani ya shilingi 370,000, mtuhumiwa mwingine alikamatwa akiwa na simu aina ya Tecno T 422 IMEI yenye thamani ya shilingi 25,000.

Alisema mtuhumiwa wa nne alikamatwa akiwa na simu aina ya ITEL ambayo imefutwa IMEI yenye thamani ya shilingi 18,000, na kwamba watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi wa awali kukamilika.

Aidha, kamanda alisema wanaendelea na operesheni maalum ya kuyakamata magari mabovu, na kuwa wameyakagua magari 637 ambapo 240 ndiyo yalikuwa mazima huku magari 367 yalikuwa na ubovu.

# Chanzo watoto kukimbilia mitaani chatajwa

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake na Watoto (WLAC), kimesema bado kuna tatizo kubwa la baadhi ya wanaume kutelekeza watoto wao na kuchangia kukatisha masomo yao na kukimbilia mitaani kujiunga katika makundi hatarishi.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa WLAC, Theodosia Muhulo, wakati wa tamasha la kutoa elimu na kuelimisha watoto kutambua na kuripoti vitendo vya ukatili lililoandaliwa na kituo hicho juzi ikiwa ni mwendelezo wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo hufanyika Juni 16, kila mwaka.

Kongamano hilo lilijumuisha shule za msingi 10 kutoka katika wilaya za Temeke na Kinondoni na liliambatana na mashindano ya uchoraji na kutoa zawadi mbalimbali kwa washindi.

Akizungumza katika tamasha hilo, Muhulo alisema wapo pia baadhi ya wazazi ambao wanashindwa kuwapatia mahitaji ya msingi watoto hao licha ya kwamba wanaishi nao nyumbani.

"Hali ya umaskini bado ni kubwa nchini, baadhi ya wanaume wanatelekeza watoto wao na kuacha wanawake wakilea peke yao na wengi wanaotelekezwa hawana uwezo wa kumudu mahitaji muhimu ya watoto," alisema Muhulo.

"Hali hii inachangia baadhi ya watoto kuacha shule na wengine kwenda kuolewa au kuanza ajira kwa ajili ya kujipatia kipato cha kujikimu. Pia wapo wanaokimbilia mitaani kuombaomba na wengine kujiunga na vikundi hatarishi."

Kwa upande wake, Leah Mbunda, kutoka Dawati la Jinsia na Watoto Kanda Maalum ya Dar es Salaam, alisema wanapokea malalamiko mengi katika dawati lao yanayohusu wanaume kutelekeza watoto wao.

"Na hapa matukio mengi ya wanaume kutelekeza watoto wao tunayoyapokea ni hasa wazazi wanapotengana, kuvunjika kwa ndoa na imekuwa sababu kubwa sana kuwaharibu watoto hawa," alisema Mbunda.

"Wakati mwingine kesi tunazozipokea unakuta ndoa inapovunjika, baba anaenda kuanzisha familia nyingine au mama naye anaenda kuolewa, kwa hiyo watoto wanaenda kuishi na bibi ambaye hana uwezo wa kuwalea."

"Kwa hiyo watoto wanatawanyika kwenda popote na inapotokea wakaangukia katika mikono isiyo salama ndiyo wengi wao wanaharibikiwa na wengine kuingia kwenye kuvuta bangi na mambo mengine mabaya."

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Kinondoni, Agnes Mbusa, alisema wazazi bado wanachangia watoto wao kufanyiwa ukatili kwa sababu wanakubaliana na watuhumiwa kumalizana kimya kimya.

"Na ndiyo maana inakuwa ni vigumu kukomesha hili tatizo kwa sababu hata tunapolifikisha kwenye vyombo vya sheria tunakosa ushahidi," alisema Mbusa.

HABARI KITAIFA

# Wanakijiji waeleza fursa kwa kufikiwa umeme

**Na Restuta Damian,** MULEBA

UPATIKANAJI wa umeme vijijini umeelezwa kuwa utasaidia kuanzisha shughuli za miradi ya ujasiriamali na viwanda vidogo, ambavyo vitainua uchumi na maendeleo ya wananchi waishio vijijini.

Hayo yalisemwa na baadhi ya wakazi kijiji cha Omurunazi, Kata ya Mushabago Wilaya ya Muleba mkoani Kagera, kwenye uzinduzi wa usambazaji wa umeme wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) awamu ya tatu mzungumko wa pili.

Shamila Abdu, alisema, wananchi wana shauku ya kupokea umeme na kuanzisha shughuli za uzalishaji wa kipato ambacho kitasaidia kuimarisha maendeleo ya familia.

Mkazi wa Kata ya Mushabago, Amon Stanslaus, alisema, uzinduzi wa umeme kufanyika vijijini umeleta matumaini ya kupanua miradi na kufanyika kijiji hapo.

"Sasa hatutapeleka tena vitu mjini kwenda kuboresha... ni muda sasa wa kufanyia hapa vijijini na kupeleka mjini kutafuta soko kwa sababu umeme ndiyo kila kitu iwe mchana au usiku," alisema Stanslaus.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa REA, Romanus Lwena, alisema katika mradi wa awamu ya tatu mzunguko wa pili hakuna kijiji ambacho kitasahaulika bila kufikiwa na umeme.

Alisema Sh. bilioni 34 zimetolewa kwa lengo la kusambaza umeme kwa mkoa wa Kagera kwenye vijiji 114 ambavyo havijapatiwa nishati hiyo.

Alisema ukamilishaji wa umeme huo kwa wananchi waishio vijijini ni Desemba 2022, kwani tayari mkoa umepokea kampuni za kandarasi zitakazofanya shughuli ya kusambazia vijiji vyote.

Akizindua mradi wa usambaziji wa umeme wa REA awamu ya tatu mzungumko wa pili kijijini Omurunazi, Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, alisema ni muda wa kila wananchi kubuni miradi na kutumia nishati na kufanya shughuli za ujasiriamali na kujiongezea kipato.




Mkuu wa Idara ya Kilimo wa Benki ya Stanbic Tanzania, Ammar Jiwaji, akizungumza wakati wa Mkutano Mkuu wa Bodi ya Kahawa mjini Dodoma, mwishoni mwa wiki. Benki hiyo imekuwa ikitoa huduma kwa wafanyabiashara katika sekta ya kilimo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC aja na dawa ya migogoro ardhi Pwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewaonya wanaohusika kuchochea migogoro ya ardhi kuacha, kwani mkoa huo sio sehemu salama tena kwao.

Kunenge alitoa onyo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizindua Baraza la Biashara la Mkoa huo, ambalo lilihudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo wawekezaji.

Alisema waliokuwa wanatajwa kuhusika na migogoro ya ardhi waache mara moja kwani wataanza kushughulikia kwa kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kunenge alisema amezungumza na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi na atamshirikisha waziri ili iundwe timu maalum itakayosimamia utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa mkoa huo.

"Tunaunda timu maalumu kuchambua maeneo yenye migogoro ya ardhi mikubwa tuanze nayo kwa kushughulikia, wenye maeneo tulinde mipaka," alisisitiza Kunenge.

Aidha, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuvamia maeneo ambayo yanamilikiwa kisheria.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) Mkoa wa Pwani, Said Mfinanga, alimweleza mkuu wa mkoa huo kuwa upo unyanyasaji unafanywa na watumishi wa TRA kuhesabu fedha kwenye droo za wafanyabiashara ambalo ni kinyume cha kazi zao.

Mkuu wa Mkoa aliagiza TRA kuacha vitendo hivyo.

# Benki UBA yawaahidi vitabu watoto yatima

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuhakikisha kila mtoto kuanzia chekechekea mpaka kidato cha nne wanapata elimu bure, Benki ya UBA Tanzania kupitia kitengo cha UBA Foundation imetoa msaada wa vitabu vya fasihi kwa vituo vya watoto yatima vya UMRA na Babu na Bibi vya mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vitabu, Mwasisi wa kituo cha UMRA Orphanage Center, Rahma Juma, alisema: "Ni muhimu kutambua mchango wa kampuni binafsi kama benki ya UBA Tanzania kwa juhudi za dhati za kuunga mkononi na kuinua sekta ya elimu nchini. Sote tunajua kwamba serikali yetu inaongozwa na sera ya serikali ya viwanda. Kwa maana hiyo hatuwezi kuwa na viwanda bila ya kuwa na wasomi wazuri kutoka kwenye jamii yetu, hiyo basi vitabu hivi vitaongeza chachu kwa watoto ambao tunawalea hapa kwani wote ni wanafunzi, hivyo kufanya vizuri katika masomo yao na hatimaye kufanikisha ndoto zao pamoja na serikali."

Rahma aliiomba Benki ya UBA na wadau wengine waendelee kuwasaidia kwenye nyaja zingine ili kuendelea kutengeneza mazingira bora kwa watoto hao kujifunza na kuongeza uelewa na kuwa na taifa lenye uweledi.

Mkuu wa Kitengo cha Digitali UBA Tanzania, Asupya Bussi, alisema wanaamini unaamini jamii iliyoelimika inajengwa kutoka katika watoto pamoja na wanafunzi kuwa na vifaa vya kufundishia vya kutosha hususani vitabu na mwamba ili kuwa na maendeleo endelevu, ni muhimu kuwekeza kwenye elimu.

Alisema Benki ya UBA imekuwa kwa muda mrefu ikisaidia sekta ya elimu nchini kwenye nyanja mbalimbali.

"Tunaamini ya kwamba msaada wa vitabu utachochea ufaulu mzuri kwa wanafunzi katika masomo yao na pia kuongeza ufaulu kwa shule zote hizi," alisema Asupya.

# Ushirika waaswa mikopo ya benki

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ameviagiza vyama vya ushirika nchini kutumia vizuri mikopo inayokopa kutoka kwenye benki mbalimbali ili ilete tija kwa wakulima wanachama badala kuitumia kwenye shughuli za uendeshaji wa miradi isiyo na tija kwa wanachama hao.

Bashe alitoa agizo hilo wakati akifunga Mkutano Mkuu wa wadau wa kahawa mwishoni mwa wiki jijini Dodoma ukihudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo wakuu wa mikoa na wilaya zinazolima kahawa, wakulima na taasisi zinazoshughulika na kilimo hicho pamoja na wafanyabiashara.

Alibainisha kuwa kwa sasa baadhi ya vyama hivyo vinapitia wakati mgumu na kukosa tija kwa wakulima kwa kuwa vimeandamwa na madeni kutoka kwa baadhi ya benki, madeni ambayo kimsingi yametokana na matumizi yasiyo na tija kwa vyama hivyo bila kuwashirikisha wanachama.

"Na hii ndio sababu vyama vya ushirika vimekuwa mzigo kwa wakulima ambao kwa sasa wanalazimika kubeba mzigo wa kulipa madeni ambayo hawajahusika kuyatengeneza." Alisema Bashe ambaye alitaka vyama hivyo kuanzia mwakani vianze kuwanufaisha wakulima badala ya kuendelea kuwekeza fedha kwenye miradi isiyo na tija.

"Mnajua haiingii akilini kabisa kuona kwamba vyama vya ushirika vinatengeneza mabilioni kupitia makato ya wakulima lakini vinashindwa kuwasaidia pale wanapokuwa na changamoto mbalimbali ikiwemo hata zile muhimu za kifamilia. Fedha zote zinaenda kulipa madeni ambayo kimsingi yamezalishwa na viongozi wanaoongoza vyama hivi kwa maslahi yao binafsi...naomba hili lifike mwisho sasa." alisema.

Akizungumzia changamoto ya matumizi mabaya ya mikopo kwenye vyama vya ushirika, Meneja wa Benki ya NBC tawi la Dodoma, Happiness Kizigira, alisema ili kukabiliana na changamoto hiyo, benki hiyo imekuwa na utaratibu wa kuendesha mafunzo kuhusu namna bora ya kutumia mikopo kabla ya kuwapatia walengwa hatua ambayo imesaidia sana kupunguza tatizo hilo.

"Pamoja na mambo mengine lengo la mikopo yetu huwa kuhakikisha tunamsaidia mlengwa kukuza mtaji wake na kufanya shughuli zake kwa ufanisi na ushindani ili atengeneze faida itakayomuwezesha kurejesha fedha kwetu bila changamoto. Hili kufanikisha hili wateja weteja wetu zikiwamo AMCOS wamekuwa wakipata mafunzo ya namna bora ya kuendesha shughuli zao kutoka kwa wataalam tunaoshirikiana nao...hii imesaidia sana."

Benki hiyo ilipata fursa ya kuelezea huduma zake mbalimbali kwa wadau hao ikiwamo huduma ya NBC Shambani inayolenga wadau wote wanaojihusisha na biashara ya Kilimo wakiwemo wasambazaji wa pembejeo za kilimo, wakulima na wasafirishaji wa mazao ya kilimo.

"Lengo hasa la huduma hii ya NBC Shambani ni kuwasaidia wadau wa kilimo kutimiza malengo yao ya biashara ya kilimo ambapo inatoa fursa kwao kuwa na akaunti ya vikundi vya wakulima kama vile AMCOS na vikundi vingine pamoja na akaunti ya mkulima mmoja mmoja," alisema.

Wakizungumzia huduma za kifedha, baadhi ya wadau wa kilimo walisema huduma hizo ni muhimu kwa kuwa kwa sasa taifa linapitia mageuzi ya kilimo biashara ambacho ustawi wake kwa kiasi kikubwa unategemea uwepo wa huduma bora za kibenki zinaenda sambamba na mahitaji wa wadau hao.

"Huduma kama NBC Shambani zinatugusa wadau wote tukiwamo hata sisi wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na usindikaji. Hii ni moja ya mfano wa huduma ambazo wadau wa kilimo tunahitaji haswa!" alisema Shakiru Kyetema, Mkurugenzi wa Kampuni ya Shayakye Trading Company inayojihusisha na uuzaji wa kahawa.

# Sababu makandarasi wazalendo kukwama hizi

**Na Joseph Mwendapole, aliyekuwa** MWANZA

MAKANDARASI wanaofanya kazi kwa ubia wametakiwa kuacha tabia ya kugawana faida kabla ya miradi wanayoifanya kukamilika, kwani hali hiyo husababisha miradi mingi kutokamilika kwa wakati.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, wakati akifunga mkutano wa nne wa mashauriano wa makandarasi Kanda ya Ziwa uliofanyika jijini Mwanza ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB).

Alisema makandarasi wengi wazalendo wamekuwa wakikwama kutokana na tamaa ya fedha mara wanapopata miradi tofauti na wenzao wa China ambao hugawana faida baaada ya kumaliza kazi na wamekuwa wakijituma kutokana na kufuatiliwa na nchi yao.

"Nimetembelea miradi mingi nchini nimekuta mingi sana wanafanya Wachina kumbe ni kwasababu wanafanyakazi kwa uaminifu na hawagawani faida mpaka kazi iishe na kwao kuna sheria kali sana wakiharibu kazi huku ndiyo sababu wana nidhamu ya kazi kuliko sisi," alisema Waitara.

Alisema tamaa na ubinafsi umesababisha makandarasi wazalendo kushindwa kuungana ili wapate uwezo wa kimtaji na mitambo ya kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi kama ilivyo kwa wenzao wa China ambao hawaweki ubinafsi mbele.

"Kuna watu wakiungana wakipata malipo ya awali tu wanapanda ndege kwenda Dar es Salaam kugawana fedha hata kabla ya mradi kuanza sasa mkifanya hivyo na mradi ukasimama fedha za kuuendeleza mtazipata wapi," alihoji Naibu Waziri.

Aidha, Waitara alisema hata kama makandarasi wataungana na kutekeleza miradi mikubwa wanapaswa kugawana faida kidogo na kuacha mtaji wa kuanzia iwapo watapata kazi zingine kwani wengi wao hushindwa kuanza miradi mipya wanayoipata.

"Kuna mtu wanashangaza sana unakuta mtu hata kazi hajafika nusu ameshanunua gari la kifahari, kamnunulia mke wake gari la kisasa mambo ya kushangaza kabisa, kwanini usisubiri ukamilishe mradi wa watu uwe na amani ya kutumia fedha zako," alisema Waitara.

Pia aliwataka makandarasi hao kurejesha fedha wanazokopa kwenye benki mbalimbali ili wajenge uaminifu na wengine waweze kukopa na kinyume chake ni kusababisha benki hizo kushindwa kuwaamini wengine wanapokwenda kukopa.

Alisema serikali itaendelea kutenga miradi ya kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo na amewataka kuonyesha uwezo kwa kukamilisha miradi watakayopewa kwa ubora wa hali ya juu na kwa wakati ili waendelee kuaminika kwa wateja.




Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka akisalimiana na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Amana, Musa Kitoi (wapili kulia), walipofika kujitambulisha ofisini kwa mkuu wa mkoa, mjini Dodoma mwishoni mwa wiki ikiwa ni baada ya Benki ya Amana kufungua tawi jipya mkoani humo. Kushoto ni Meneja wa Tawi la Amana Dodoma, Athumani Julius na Meneja Masoko, Dasu Musa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mpango aipa NMB changamoto ya gawio

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya NMB imetoa gawio la Sh. bilioni 21.8 ikiwa ni ongezeko la asilimia 43 ya gawio la mwaka jana ambalo lilikuwa Sh. bilioni 15.25, huku Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiipa changamoto kuongeza gawio zaidi.

Akipokea mfano wa hundi mwishoni mwa wiki, Dk. Mpango, alisema kiasi hicho kimemridhisha kwa mwaka huu, lakini akataka waongeze maarifa zaidi ili kutoa gawio la juu ikiwamo kuwekeza katika nchi jirani.

Dk. Mpango alisema kiwango kilichotolewa mwaka jana hakikumfurahisha, hivyo aliagiza lazima waongeze juhudi.

Gawio lililotolewa jana ni sehemu ya faida ya Sh. bilioni 206 ambazo benki hiyo ilipata katika msimu wa kuishia Desemba 2020 baada ya kuondoka kodi.

Serikali inapokea gawio hilo kutokana na umiliki wake wa hisa asilimia 31.8 ndani ya benki hiyo.

"Nimefurahishwa sana na hiki mlichotoa, pamoja na mafanikio haya lakini nataka mwongeze ubunifu ili mwaka muwe zaidi ya hapa, hata hivyo nakuagiza Waziri wa Fedha kwamba kiasi hiki kikafanye kazi nzuri kwa wananchi ambayo imekusudiwa," alisema Dk. Mpango.

Aliwataka kushirikiana na taasisi zingine ili wakae na Benki Kuu (BoT) kujadili kuhusu riba kubwa ambayo bado inatozwa na mabenki, hivyo kusababisha watu washindwe kukopa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NMB, Dk. Edwin Mhede, alisema fedha hizo zilishawekwa katika akaunti ya Msajili wa Hazina, na kwamba mwakani watakuwa na kiasi kikubwa zaidi kutokana na mwenendo wanavyoona.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema mbali na gawio hilo, lakini wamelipa serikalini Sh. bilioni 2.45 kama kodi za tozo mbalimbali na kutumia asilimia moja ambayo ni zaidi ya Sh. bilioni 2 kwenye huduma za kijamii.

Alisema benki hiyo imefikia mtaji wa Sh. trilioni 1.1 kutoka Sh. bilioni 660 kwa mwaka 2015 hivyo ukuaji wake unatia matumaini kwamba itaendelea kuwa ni benki bora yenye kutoa huduma kwa viwango vinavyotakiwa.

Nipashe
# Spotika



MAGOLIKIPA 10 BORA MSIMU HUU 2020 -21 UK. 12 - 13




# REKODI 5 ZA KUVUNJWA NA RONALDO EURO 2020

**LISBON,** Ureno

JINA la Cristiano Ronaldo limejaa rekodi ya kila aina kwenye soka na sasa linatajwa kuvunja rekodi nyingine katika michuano ya Euro 2020 inayoendelea.

Katika umri wa miaka 36, Euro 2020 inaweza kuwa michuano yake ya mwisho mikubwa katika kipindi cha uchezaji soka cha Ronaldo.

Kwa mchezaji ambaye ametawala soka kwa kipindi cha muongo mmoja na nusu, kuvunja rekodi si jambo jipya kwake.

Licha ya umri wake, Ronaldo ni mmoja wa wafungaji bora wa wakati wote wa ligi kubwa tano za Ulaya msimu huu. Pia ameshinda Kiatu cha Dhahabu kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, kwa kumzidi mabao matano Romelu Lukaku.

Aliisaidia Ureno kushinda taji la Euro mwaka 2016 na kwa sababu ya ubora wa kikosi chake, pia wana nafasi kubwa kwenye michuano hii ya Euro 2020.

Makala haya yanaangalia rekodi tano zinazoweza kuvunjwa na Ronaldo kwenye Euro 2020, twende sasa...

### #5. FAINALI NYINGI ZAIDI

Ronaldo alianza kucheza michuano ya Euro mwaka 2004 na ameendelea kuwa mchezaji muhimu kwa Ureno tangu wakati huo. Ametawala dunia ya soka kwa kushinda mataji mengi. Ronaldo aliiongoza Ureno kushinda taji la Euro 2016 katika fainali dhidi ya Ufaransa.

Pamoja na michuano hii, Ronaldo amecheza mashindano ya Euro mara tano hadi sasa. Wachezaji 17 wamecheza michuano ya Euro. Lakini hakuna aliyecheza mara tano.

Na sasa wakati Ureno inapocheza michuano hii ya Euro 2020, Ronaldo amekuwa mchezaji wa kwanza kucheza kwa mara ya tano michuano hiyo.

### #4. MABAO MENGI KWENYE EURO

Ronaldo alifunga bao lake la kwanza la michuano ya Euro dhidi ya Ugiriki akifunga hatua ya makundi wakati wakishinda 1-0. Tangu hapo Ronaldo amefunga mabao mengine jumla 11 ikiwa ni pamoja na matatu aliyofunga katika mashindano haya kwenye michuano ya Euro. Na sasa anatarajiwa kuongeza mengine zaidi.

Kwa sasa ameipiku rekodi ya Michael Platini ya kufunga mabao mengi (nane) kwenye michuano hiyo. Cha kufurahisha ni kwamba mabao yote tisa ya Platini aliyafunga wakati wa michuano ya Euro 1984. Ronaldo aliifikia rekodi ya Platini kwa kufunga katika michuano minne kabla ya kuipiku. Hivyo kwa sasa Ronaldo ndiye mchezaji wa kwanza katika historia ya mashindano hayo kufunga mabao mengi zaidi.

### #3. MECHI NYINGI EURO

Gwiji Gianluigi Buffon ndiye aliyekuwa akishikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi kwenye mashindano hayo, ikiwamo hatua ya kufuzu.

Raia huyo wa Italia amecheza jumla ya mechi 58 kwa timu ya taifa. Buffon alistaafu kuichezea timu ya taifa mwaka 2017.

Ronaldo kabla ya michuano hii alikuwa amecheza jumla ya mechi 56 za Euro, ikiwamo kwenye kufuzu na hatua ya makundi. Na katika michuano ya hii ya Euro 2020, ameshacheza mechi tatu ambazo zinamfanya kuivunja rekodi hiyo ya Buffon kwa kufikisha mechi 59. Katika mechi hizo 59, Ronaldo ameshinda 38, akitoka sare 12 na kufungwa tisa.

### #2. UMRI MKUBWA KUFUNGA

Ureno imetawala soka la Ulaya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Walishinda taji la mashindano ya Euro mwaka 2016, na baadaye wakashinda taji la Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Na sasa pia Ureno wanapewa nafasi kubwa ya kushinda taji la Euro 2020 na Ronaldo kama akifunga bao atakuwa mchezaji mwenye umri mkubwa zaidi kufunga katika fainali hizo.

Kwa sasa rekodi hiyo inashikiliwa na nyota wa zamani wa iliyokuwa Ujerumani Magharibi, Bernd Hölzenbein, aliyoiweka mwaka 1976. Kama Ureno itatinga fainali Ronaldo siku hiyo atakuwa na umri wa miaka 36 na siku 156.

### #1. MABAO MENGI YA KIMATAIFA

Ronaldo anakaribia kuweka rekodi ya ufungaji wa wakati wote kwenye mechi za kimataifa. Rekodi hiyo inashikiliwa na nyota wa zamani wa Iran, Ali Daei, ambaye amefunga mabao 109 ya kimataifa kwa jina lake. Ronaldo anakaribia kuifikia akiwa na mabao 106.

Sasa anahitaji mabao manne tu kuweza kuipiku rekodi hiyo ya Ali Daei.

Wachezaji wanaomfuatia Ronaldo ambao bado wanacheza ni Ali Makhbout wa Falme za Kiarabu na Lionel Messi wa Argentina wenye mabao 73 kila mmoja wakifuatiwa na Sunil Chhetri wa India aliyecheka na nyavu mara 72.

Kama Ronaldo anaweza kufunga mabao manne ukiacha matatu ambayo ameshafunga hadi sasa kwenye michuano hii ya Euro 2020, atavunja rekodi hiyo na kuwa mchezaji aliyeifungia mabao mengi zaidi timu yake ya taifa duniani.

## ISIKUPITE

KIPA wa Paris Saint-Germain, Keylor Navas ndiye anayeongoza kwa kuokoa michomo mingi ya hatari ya mabao kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, akifanya hivyo mara 54, akifuatiwa na Manuel Neuer wa Bayern Munich (35), Édouard Mendy wa Chelsea (31), Agustín Marchesín wa FC Porto (29) na Thibaut Courtois wa Real Madrid (26).



# MAGOLIKIPA 10 BORA MSIMU HUU 2020-21



NEUER

**LONDON,** England

MAGOLIKIPA ni miongoni mwa wachezaji wanaopewa lawama kubwa baada ya timu kuwa na kiwango kibovu dimbani. Katika soka la kisasa kazi ya kipa ni zaidi ya kulinda goli kwani pia wanakuwa na nafasi ya kuanzisha mashambulizi.

**Makala haya inawaangalia magolikipa 10 bora, ambao wamekuwa na mchango mkubwa wa kuzisaidia timu zao kupata pointi msimu huu uliomalizika wa 2020/21.**

### #10. ANTONIO ADAN | SPORTING LISBON

Antonio Adan alikuwa na wakati wa kuvutia sana msimu huu.

Kipa huyo wa zamani wa Real Madrid na Atletico Madrid, alihamia mji mkuu huo wa Ureno kipindi cha majira ya joto kilichopita, na katika msimu wake wa kwanza amewasaidia 'Leoes' hao kushinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka 19.

Alikuwa mchezaji muhimu kwa Sporting akiruhusu mabao 20 tu kutikisa nyavu zake kwa msimu wote na alicheza mechi 19 bila kuruhusu bao kati ya 33 kwa klabu hiyo.

### #9. SAMIR HANDANOVIC | INTER MILAN

Tuna mshindi mwingine wa Ligi akiwa na Inter Milan, Samir Handanovic katika orodha yetu akiwa nafasi ya tisa. Golikipa huyo mkongwe amekuwa na Milan tangu mwaka 2012 na hili ndilo taji lake kubwa na klabu hiyo.

Kama Adan, kiwango cha Handanovic pia kiliisaidia Inter kushinda taji lake la kwanza la Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka 11. Handanovic anaongoza kwa nyavu zake kutotikiswa kwenye Serie A, aliruhusu mara 14 tu katika mechi 36 msimu huu.

### #8. KOEN CASTEELS | WOLFSBURG

Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, inajulikana kwa kuzalisha makipa bora na wa daraja la juu duniani. Manuel Neuer, Marc-André ter Stegen ni miongoni mwa zao la makipa wa sasa, huku Jens Lehmann na Oliver Kahn ni makipa ambao walikuwa kwenye kiwango cha juu kwa miaka yao.

Mmoja wa magolikipa ambao wapo kwenye rada ni kipa namba moja wa Wolfsburg, Koen Casteels. Nyota huyu wa kimataifa wa Ubelgiji hajaruhusu nyavu zake kutikiswa katika mechi 14 kwa Wolves msimu huu wakati walipopata nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa ni mara ya tatu kwenye historia yao.

Kati ya Januari na Machi, alicheza dakika 673 bila kuruhusu bao kwenye mechi za ligi, na kuisaidia Wolfsburg kuwa timu ya pili yenye safu imara ya ulinzi kwenye Ligi Kuu. Katika mashindano yote, alikuwa na kiwango cha kuvutia akiokoa hatari kwa asilimia 71.

Bahati mbaya hajaitwa kwenye kikosi cha Ubelgiji kinachoshiriki michuano ya Mataifa ya Ulaya, Euro 2020, baada ya kufanyiwa upasuaji.

### #7. EDOUARD MENDY | CHELSEA

Kuna wakati golikipa unaweza kuwa na bahati kwa klabu na ilikuwa hivyo kwa Chelsea baada ya kumsajili Edouard Mendy kwa pauni milioni 22 na amekuwa msaada mkubwa kwao msimu huu.

Kipa hiyo raia huyo wa Senegal mwenye umri wa miaka 29, alisajiliwa kwa ajili ya kuchukua mikoba ya Kepa, kipa ghali zaidi Ulaya.

### #6. EMILIANO MARTINEZ | ASTON VILLA

Mara zote inavutia kuona magolikipa ambao walikuwa chaguo la pili kwenye klabu zao wakienda kuwa mashujaa kwingine. Golikipa wa zamani wa Arsenal, Emiliano Martinez alikuwa na msimu bora kabisa katika mwanzo wake pale Aston Villa na kiwango chake kimeisaidia sana klabu hiyo msimu huu.

Raia huyo wa Argentina, aliondoka kwa 'Washikabunduki' hao wa London na kwenda Aston Villa kipindi cha majira ya joto kilichopita na amecheza katika kila mechi. Anashika nafasi ya tatu kwa kutoruhusu nyavu zake kutikiswa katika mechi 15.

Na sasa anapambana kuwa chaguo la kwanza kwa kikosi cha Argentina katika michuano ya Copa America.

### #5. MIKE MAIGNAN | LILLE

Mike Maignan ni mmoja wa makipa ambao wamecheza mechi nyingi bila kuruhusu mabao katika Ligi Kubwa tano za Ulaya. Kipa huyu wa Lille alifurahia msimu mzuri akiruhusu mabao 23 na akicheza mechi 21 bila nyavu zake kutikiswa.

Na alikuwa na mchango mkubwa kwa Lille wakati wakibeba taji la Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, msimu huu na ni zao la akademi ya Paris Saint-Germain.

### #4. MANUEL NEUER | BAYERN MUNICH

Orodha hii isingekamilika bila jina la Manuel Neuer, bila shaka yoyote ni mmoja wa makipa bora wa wakati wote. Ingawa ni golikipa bora wa FIFA mwaka 2020, alikuwa na mechi tisa tu ambazo hakuruhusu bao msimu huu, na alishindwa kufikia rekodi ya Oliver Kahn ya kucheza mechi nyingi bila kuruhusu nyavu kutikiswa kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga kwa msimu mmoja.

Katika umri wake wa miaka 35, bado anaonekana ana nguvu ya kuendelea kucheza kwa misimu mingine inayokuja. Msimu huu ameruhusu mabao mengi zaidi tangu alipojiunga hapo Bayern Munich mwaka 2011.

### #3. THIBAUT COURTOIS | REAL MADRID

Thibaut Courtois amejithibitisha yeye mwenyewe kama mmoja wa makipa bora kabisa duniani kwa klabu na nchi yake. Amekuwa na uwezo mkubwa wa kuokoa hatari langoni mwake na kuisaidia Real Madrid msimu huu wa 2020-21.

Licha ya kuwa na asilimia kubwa ya 81.1 kuokoa hatari langoni mwake kwenye LaLiga, lakini yeye pamoja na wachezaji wenzake walimaliza msimu bila taji lolote.

Alicheza mechi 17 bila kuruhusu bao na alifungwa mara 28 katika mechi 38.

Alikuwa na kiwango kizuri kwenye mchezo wa ushindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool na aliokoa hatari nyingi wakati Real Madrid wakifungwa na Chelsea kwenye nusu fainali.

### #2. EDERSON | MANCHESTER CITY

Watu wengine wanasema kwamba, Ederson ni golikipa mwenye bahati kwani yupo katika moja ya safu ya ulinzi ghali zaidi pale Manchester City, lakini ana uwezo mkubwa wa kuhimili kila kitu langoni.

Wakati akiwa bize kuokoa hatari langoni mwake, lakini alikuwa akianzisha mashambulizi kwa wachezaji wenzake.

Alishinda tuzo ya kipa bora ya "Golden Glove" baada ya kucheza mechi 18 bila kuruhusu bao na muhimu zaidi ni pale alipoanzisha shambulizi la Gundogan Februari na pengine lingekuwa tukio bora zaidi la msimu kama Alisson asingepiga kichwa kufunga dhidi ya West Bromwich Albion na kuisaidia Liverpool kupata ushindi.

### #1. JAN OBLAK | ATLETICO MADRID

Golikipa anahukumiwa kutokana na uwezo wake wa kutoruhusu nyavu zake kutikiswa na kuokoa hatari nyingi za kufungwa mabao langoni mwake.

Hakuna aliyefanya kazi kubwa zaidi ya hiyo kama kipa wa Atletico Madrid, Jan Oblak.

Kipa huyo raia wa Slovenian alitwaa tuzo ya Zamora na pia aliongoza kwa kucheza mechi nyingi bila nyavu zake kutikiswa. Na pia amefungwa mabao machache kwenye ligi.

Ni mwokoaji mzuri wa penalti, na aliokoa mbili kati ya nne alizopigiwa msimu huu.

Ingawa yeye si mtoaji pasi kama Ederson, lakini ana mchango mkubwa zaidi wa kuokoa hatari yoyote langoni mwake. Na kwa kiasi kikubwa aliisaidia sana Atletico kushinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu huu.

## Nukuu

"Sina haraka ya kuiongoza Barça. Ni kweli kwamba tayari nilishasema hapana mara mbili, lakini sijisikii tayari bado. Haukuwa wakati, kwa sababu nyingi. Hivi sasa, mimi ninafuraha hapa Al Sadd. Kusema hapana ni uamuzi mgumu zaidi niliyopaswa kuuchukua, lakini sidhani kama hiyo ilikuwa wakati mwafaka kufanya hivyo," **nyota wa zamani wa Barcelona, Xavier Hernández**



"Nafikiri mwaka huu nimekuwa mwenye wakati mgumu. Nafikiri ni wakati wa kutumika kwenye klabu kwa mkataba wa muda mrefu na kuwa na wakati wa kuonyesha kiwango changu. "Barcelona? Hapana, hicho si kipaumbele changu, mimi nafikiria zaidi kubaki Real Madrid na si vinginevyo," **Kiungo wa Arsenal, Dani Ceballos anayeichezea kwa mkopo akitokea Real Madrid.**



"Nafikiri wachezaji kama Jordan Henderson na Harry Kane, wametoa mchango mkubwa sana kwa kukua kwangu nje na ndani ya uwanja. Wamekuwa msaada mkubwa na nimejifunza mengi kwao, hivyo naamini nitaendelea kukua chini yao," **Kiungo wa Aston Villa na timu ya Taifa ya England, Jack Grealish**





# AZAM INAVYOZIPIGA BAO SIMBA, YANGA

DUBE

**Na Adam Fungamwango**

ACHANA na kumsajili beki wa kushoto wa Ruvu Shooting, Edward Manyama kwa mkataba wa miaka mitatu na kuzipiga bao klabu ya Simba na Yanga zilizokuwa zikimnyemelea, klabu ya Azam FC imekuwa pekee nchini inayoongezea mikataba wachezaji wake inayowahitaji kabla ya kukaribia kumalizika.

**Ukiona mchezaji yeyote kwenye klabu ya Azam anakaribia kabisa kumaliza mkataba wake na uko ndani ya miezi sita, basi inawezekana kabisa kuwa huyo hahitajiki.**

Klabu hiyo imekuwa na utaratibu mzuri wa kuwaongezea mikataba wachezaji wao wakiwa bado wana mikataba mirefu, kitu ambacho mara nyingi kinawaepusha na purukushani, migogoro au tetesi za wachezaji wao wakuchukuliwa na klabu zingine.

Ni mara chache sana Azam kuchukuliwa mchezaji ambaye bado inamhitaji, kwa sababu wengi wanakuwa na mikataba mirefu na ikikaribia mwaka mmoja au miezi zaidi ya sita, wanamwongeza iwapo watamhitaji.

Kosa ambalo halitosahaulika la Azam ni la mwaka 2017 ilipowaachia wachezaji Erasto Nyoni, Shomari Kapombe, John Bocco na Aishi Manula hadi mikataba yao ilipomalizika na hii ilitokana na kubadilisha sera yao ya usajili, ikitaka kusajili vijana zaidi.

Wakati ikiwa kwenye mazungumzo na wachezaji hao nia ni kutaka kupunguza kiwango cha mshahara, wachezaji hao walitimkia Simba na tangu wakati huo wamekuwa wakipa ubingwa kwa misimu mitatu mfululizo.

Tangu wakati huo, Azam haikurudia tena kosa kama hilo. Kwenye makala haya tutaangalia baadhi ya wachezaji ambao wameongezewa mikataba na klabu hiyo bila kelele, wala shinikizo la mchezaji kutaka kuhamia klabu nyingine, haya sasa...

### #1. BRUCE KANGWA

Ilikuwa Machi mwaka huu, Azam FC ilipomwongeza mkataba wa mwaka mmoja beki wa kushoto wa klabu hiyo, Bruce Kangwa raia wa Zimbabwe. Huyu ndiye atakuwa anasaidiana na Manyama. Kangwa aliongezewa mkataba huo, huku ule wa awali ukitarajiwa kumalizika Agosti mwaka huu, yaani mwisho wa msimu huu.

Lakini baada ya kuongezwa, sasa Kangwa atasalia hadi 2022 na kama kiwango kitaendelea kuridhisha huenda akaongezwa tena kama ulivyo utaratibu wa klabu hiyo.

### #2. SELEMANI IDD 'NADO'

Selemani Idd 'Nado', anayecheza kama winga, wakati mwingine kama kiungo mshambuliaji, Aprili mwaka huu aliongezewa mkataba wa miaka miwili na Azam FC.

Nado sasa atahudumu kwenye klabu hiyo hadi 2024, hivyo kutokuwa na wasiwasi wa klabu yoyote kuthubutu kumng'oa bila kutoa pesa ya maana.

Mchezaji huyo alijiunga na Azam FC mwaka 2019, akitokea Mbeya City baada ya kung'ara kwenye michezo ya mchangani 'Ndondo Cup'. Kwa sasa licha ya kuwa tegemeo Azam FC, lakini yupo kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars.

### #3. PRINCE DUBE

Nadhani huyu ndiye atakuwa mchezaji pekee ambaye Azam ilitikiswa kidogo licha ya kuwa ana mkataba na timu hiyo. Raia huyu wa Zimbabwe kwa sasa ndiye kinara wa mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Dube, ambaye amejizolea sifa kubwa nchini kutokana na umahiri wa upachikaji mabao, ulisababisha mpaka kuwa na tetesi kwamba kuna baadhi ya timu wanataka kumnunua. Klabu za Simba, Yanga nyingine za Afrika Kusini na Misri, zikaelezwa kumnyemelea.

Ilichofanya sasa Azam FC pamoja na kuwa mkataba mrefu, Juni Mosi, mwaka huu ilimwongeza tena mkataba wa miaka miwili, akiwa amejifunga hadi 2024.

### #4. AYOUB LYANGA

Mwezi Juni mwaka huu tena, Azam FC ilimwongeza mkataba winga wake machachari, Ayoub Lyanga na sasa atasalia Chamazi Complex hadi 2024. Awali Azam FC ilimsajili winga huyo msimu uliopita kutoka Coastal Union, lakini imeamua tena kumwongeza miwili tena ili kusiwe na uwezekano ya klabu yoyote ndani na nje ya nchi kuanza kumnyemelea.

Yeyote anayemtaka atalazimika kuiona kwanza klabu yake na kutajiwa dau halisi la mchezaji huyo, kabla ya kumsajili.

### #5. BRYSON RAFAEL

Mchakato wa kumsainisha Manyama kwenye klabu ya Azam FC, uliendа pamoja na wa kumwongezea mkataba kiungo mkabaji wao, Bryson Rafael.

Ni mchezaji ambaye msimu huu ameonekana kung'ara sana akiwa na kikosi hicho, hivyo kumpa mkataba mapema kabla ya kuanza kunyemelewa.

Yeye atasalia kwenye klabu hiyo hadi 2023, na kama akiendelea kuonyesha uwezo huenda Azam ikaazimia kumwongeza tena.

## JE, WAJUA?



KIUNGO Thomas Partey kwa sasa ni mshindi wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga kwa msimu wa 2020/21, kwani mechi tatu alizowachezea mabingwa Atletico Madrid kabla ya kujiunga na Arsenal kwa dau la pauni milioni 45, zinatosha kutambulika kama mchezaji aliyeibebesha ubingwa timu hiyo.



# Kabudi ataka kuimarishwa kwa ofisi ya wakili mkuu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema kuwa ipo haja ya kuimarishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kusaidia kusimamia mashauri yote yanayoikabili serikali ya ndani na nje ya nchi.

Hatua hiyo, itasaidia kuiondoa serikali mzigo wa gharama ambazo imekuwa ikitumia kuwalipa mawakili wa nje ya nchi.

Waziri Kabudi aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akitoa hotuba yake ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Alisema ipo haja kwa serikali kuendelea kuboresha utendaji kazi wa ofisi hiyo ili kusadia kusimamia kesi zote za serikali za ndani na nje ya nchi.

Kabudi alisema hali hiyo itasaidia taifa kuondokana na matumizi makubwa ya fedha kwa ajili ya kulipa mawakili wa nje pale taifa linapofunguliwa kesi nje ya nchi.

"Hawa viongozi wetu wanapata shida sana unakuta wametenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kuwekeza kwenye miundombinu au miradi ya maendeleo lakini unakuta nchi inashtakiwa na kwenda mahakamani unatakiwa kutumia fedha nyingi sana kulipa mawakili," alisema Prof. Kabudi.

Pia alisema kuwa kesi ambazo zimekuwa zikifunguliwa zinailazimu nchi kulipa mamilioni ya fedha ambayo yangetumika katika miradi mingine ya maendeleo.

"Hivi sasa tuendelea tu na hiki kipindi cha mpito, lakini baadaye nataka ofisi hii ndiyo iwe inasimamia kesi zote za serikali za ndani na nje tutafanikiwa tuu kama tutaendelea kuimarisha Ofisi hii ya Wakali Mkuu wa serikali," alisema.

Kadhalika, alisema ipo haja ya kuwa na taasisi ya mafunzo ya mawakili wa ofisi ya serikali ambayo itatumika kutoa mafunzo ya mara kwa mara ili kuimarisha utendaji kazi wao.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, alisema kuwa pamoja na mafanikio waliyoyapa ikiwamo kuokoa fedha za serikali lakini bado wanakabiliwa na kero nyingi ikiwamo idadi ndogo ya watumishi.

Malata, alisema kuna tatizo la uhaba wa vitendea kazi ikiwamo magari katika ofisi zao 16.



Mbunge wa Jimbo la Chamwino, Deogratius Ndejembi (wapili kulia) akifurahia na wananchi wa jimbo lake baada ya kuwakabidhi mifuko 1,136 ya saruji yenye thamani zaidi ya Sh. milioni 20.1 mwisho wa wiki Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ugonjwa wa kisukari watajwa tishio kubwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

IMEELEZWA kuwa watu 10 kati ya 100 wana tatizo la ugonjwa wa kisukari huku asilimia 60 ya wagonjwa wakiwa hawajui kama wanaumwa.

Mkurugenzi Msaidizi Kitengo cha Magonjwa yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. James Kiologwe, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa waganga wakuu na waratibu wa magonjwa yasiyoambukiza. Alisema asilimia tisa ya wagonjwa hao wanatatizo kubwa ka kisukari.

Aidha, alisema magonjwa ambayo yasiyo ya kuambukiza yamekuwa yakiongezeka nchini na takwimu zinaonyesha kwamba watu 26 kati ya 100 wana matatizo ya shinikizo la juu la damu.

"Watu 36 hadi 22 wana mafuta mengi katika mishipa yao ya damu na zaidi ya robo tatu ya watu wenye shinikizo la juu la damu hajijui kama wana tatizo hilo unasikia tu mtu amenguka hajijui," alisema.

Hata hivyo, alisema matatizo hayo yamekuwa yakiongezeka kwa Watanzania hivyo kupunguza kasi ya maendeleo ya nchi.

"Kila asilimia 10 ya ongezeko la magonjwa haya yamekuwa yakipunguza pato kwa asilimia 0.5, maana yake ni kwamba tutakuwa hatuna nguvu kazi ya kutosha katika maendeleo pamoja na gharama kubwa ya matibabu kwa wagonjwa," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema wizara imekuja na mpango wa kuhakikisha matatizo hayo yanapungua kwa kuja na mpango wa kubadili mtindo wa maisha.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Dk. Ntuli Kapologwe, aliwataka waratibu wa afya katika mikoa kusimamia zoezi la kupambana na magonjwa yasiyokuwa yakuambukiza.

Alisema lazima wataalamu hao watoe elimu kuhusu jinsi ya kula milo kwa kuwa wengi wamekuwa wakipotoshwa.

"Kwa sasa tuna miongozo kama sita wa kwanza ni usimamizi wa vituo vya kutolea huduma kwa kutumia kamati kwenye ngazi wa kituo, mpango wa maendeleo wa afya ya msingi awamu ya pili," alisema.

Naye Katibu Mkuu Chama cha Wagonjwa wa Kisukari, Prof. Kaushik Ramaiya, alitaja magonjwa manne ambayo yamekuwa hatari kwa sasa ni sukari, moyo, mapafu na saratani.

Alisema ili kukabiliana na magonjwa hayo ni lazima watu wafanye mazoezi kwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya magonjwa sio ya kuambukiza yanazuilika.

# Wabunge waingilia kati kupungua samaki Mtera

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji imewataka wavuvi katika Bwawa la Mtera kudhibiti uvuvi haramu kwa kuwa unasababisha kupungua kwa samaki kwenye baadhi ya maeneo.

Aidha, imeridhishwa na elimu iliyotolewa kuhusu uvuvi haramu kwa wavuvi hao.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, aliyasema hayo jana baada ya kufanya ziara katika kijiji cha Msisiri wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma na Kijiji cha Mnadani Wilaya ya Iringa na kuzungumza wavuvi na wananchi wa maeneo hayo.

Alisema katika vijiji vyote walivyopita wamekuta wavuvi na wananchi wanayo elimu hiyo na wanashiriki katika kudhibiti kwa kukamata nyavu haramu na kuziteketeza.

"Kwa kweli sisi kamati baada ya kuzungumza na wananchi pamoja na wavuvi wa maeneo yote hayo mawili tuliyotembelea tumeridhishwa na elimu iliyotolewa kuhusu uvuvi haramu kwa wavuvi wa Bwawa la Mtera," alisema.

Kadhalika, aliwaahidi wananchi wa Kijiji cha Mnadani kuwa atalifikisha tatizo la wingi wa viboko katika bwawa hilo kwa Waziri wa Maliasili na Utalii ili kulishughulikia.

Kwa upande wake, Katibu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayeshughulikia Sekta ya Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, alisema wizara imekuwa ikitoa elimu kuhusu uvuvi haramu na madhara yake kwa wavuvi na wananchi wanaolizunguka bwawa hilo.

Alisema hatua hiyo imesaidia kudhibiti na kuteketeza nyavu zisizofaa zilizokamatwa.

Dk. Tamatamah aliwaahidi wavuvi wa kijiji cha Msisiri kuwaletea injini moja ya boti mwezi Julai, 2021 ambayo pamoja na shughuli za uvuvi itawasaidia kufanya doria za kudhibiti uvuvi haramu.

Aidha, alisema atatuma wataalamu wa utafiti kutoka TAFIRI kuangalia kutafiti kama upo uwezekano wa kuweka mbegu ya samaki ili kusaidia kuongeza wingi wa samaki kwenye bwawa hilo.

Aliwataka wavuvi kujiunga kwenye vyama vya ushirika ili kukopesheka na kupata zana sahihi za uvuvi zinazotolewa na wizara.

Naye Mkazi wa Kijiji cha Mnadani, Kata ya Izazi wilayani Iringa, Amiri Kiselo, aliiomba serikali kusaidia kukabiliana na ongezeko la viboko kwenye bwawa hilo ambao wanasababisha wavuvi kuhofia kuvua samaki.

"Tatizo hili limefanya samaki kuwa wachache katika masoko na kuwafanya wavuvi kutafuta shughuli nyingine za kuwaingizia kipato tunaomba kamati mtusaidie," alisema.



## Wazazi, walezi wakumbushwa wajibu wa masomo

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalibu Lubandamo, amewataka wazazi na walezi wilayani humo kuwa mstari wa mbele, kuhakikisha wanatimiza mahitaji muhimu ya watoto wao wakati wa masomo.

Miongoni mwa mahitaji hayo ni ununuzi wa sare za shule na uchangiaji wa michango ya shule.

Lubandamo alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na watendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo Rujewa, ambapo alisema kauli ya elimu bure imebadilisha mitazamo ya wananchi na kusahau kuhudumia mahitaji ya watoto wao.

Alisema wazazi wengi wamejikita kwenye shughuli za uzalishaji mali na kusahau jukumu la kuwahudumia watoto hao na kuchochea kujiingiza kwenye vitendo visivyofaa kwenye jamii na kuharibu ndoto zao.

"Dhana ya elimu bila malipo imepokelewa vibaya na baadhi ya wazazi kwani hawasikii wala kuelewa jambo lolote linalohusu michango ya shule kama vile madawati, wanamtuma mtoto shule bila daftari wala sare za shule kwa madai kuwa atazikuta huko huko serikali itamnunulia," alisema Lubandamo.

Katibu Tawala la Wilaya ya Mbarali, Michael Semindu, alisema mikakati ya wilaya hiyo ni kuhakikisha tatizo la vyumba vya madarasa inashughulikiwa na kwamba itakuwa historia kwani tayari wamekwisha aanza kuwahamasisha wananchi kuchangia.

Alisema kwa mwaka wa masomo wa 2020/2021 ni madarasa 46 yamejengwa katika wilaya hiyo wakati hitaji ni madarasa zaidi ya 100 kwa mwaka wa masomo ujao.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa, Chameta Godigodi, alisema mamlaka hiyo inakabiliwa na vikwazo mbalimbali ikiwamo kutokamilika kuwa mamlaka kamili hivyo kushindwa kutatua baadhi ya mahitaji.

# Wataka watoto wenye ulemavu mguu kifundo kusaidiwa matibabu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda ya Mbeya (MZRH), imehamasisha taasisi, wafanyabiashara na wadau wengine kuchangia matibabu kwa watoto wenye ulemavu wa mguu kifundo.

Lengo ni kuwa na uhakika wa matibabu ukilinganisha na ilivyo sasa ambapo gharama ni kubwa.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, wakati akizungumza na Nipashe, ambapo alisema huduma ya matibabu kwa watoto wenye ulemavu wa mguu kifundo inahitaji michango ya kifedha kutoka kwa wadau mbalimbali ili kupata matibabu.

Alisema hospitali hiyo inaendelea kutoa matibabu ya mguu kifundo, na kwamba ili kuwatibu kwa wakati wenye matatizo, ni vyema wadau wakasaidia michango ya fedha kwa kuwa asilimia kubwa hawana uwezo wa kujigharamia.

"Tunahitaji msaada wa fedha kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye ulemavu wa mguu kifundo, asilimia kubwa ya wanaofika hawawezi kumudu gharama za matibabu, hivyo wadau tunahitaji mtusapoti, wanahabari mtusaidia kuhamasisha," alisema Dk. Mbwanji.

Aidha, aliwaomba viongozi wa dini kuhamasisha waumini kuchangia matibabu hayo, wanasiasa kuhakikisha watoto wanaozaliwa wakiwa na ulemavu wa miguu kifundo wanapozaliwa wapelekwe katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya.

Mratibu wa Mguu Kifundo, Nyanda za Juu Kusini, Veronica Marishay, alisema jumla ya watoto 463 wenye matatizo ya mguu kifundo wamepatiwa matibabu tangu mwaka 2015 hadi sasa kwa ushirikiano na Shirika la TCCO katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya.

Aliongeza kuwa hospitali hiyo kwa kushirikiana na hospitali binafsi wamehudumia watoto wapatao 1,450 hadi sasa.

Aliwahamasisha wazazi kuwapeleka watoto kwenye matibabu wanapobainika kuwa na mguu kifundo na kuacha imani za kishirikina ili wapate matibabu kwa wakati.

Akitoa ushuhuda wa mtoto wake ambaye alizaliwa na ulemavu wa miguu kifundo, Stephano Simfukwe, alisema kuwa alianza matibabu mfululizo kwa kipindi cha miaka mitano mpaka sasa mtoto amepona.




Mwenyekiti wa Jukwaa la Watoto mkoani Mbeya, Eva Mwasongwe, akisoma risala kwa Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya (hayupo pichani), Dk. Angelina Lutambi, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika ambayo kimkoa yalifanyika Kata ya Ipinda wilayani Kyela. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wakulima wa Songwe wataka elimu ya sumu kuvu

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

WAKULIMA katika Kijiji cha Ivwanga, Kata ya Mlowo mkoani Songwe, wamewaomba maofisa kilimo kuwafundisha namna ya kutenganisha mahindi yenye sumu kuvu na mahindi masafi ili kulinda soko la kimataifa.

Wamesema wamekuwa wakipata hasara wanapopeleka mahindi sokoni kwa sababu hayauziki, hivyo wameomba maofisa kilimo kuwapatia elimu ya namna ya kuzalisha pia kutenganisha yenye sumu kuvu na safi ili kupata soko la uhakika.

Kutokana na tatizo hilo, miongoni mwa kampuni kama ilivyo Ekari Moja Tanzania imechukua jukumu la kufundisha kutenganisha mahindi yenye sumu kuvu na masafi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi kwenye shamba darasa lililopo katika kijiji cha Ivwanga, mkulima wa Kijiji cha hicho, Joseph Mwampashi, alisema kuwa akivuna mahindi shambani huchambua yaliyo mabovu au sumu kuu na kuyatenga na kubaki mahindi bora ambayo huhifadhi kwa kutumia mifuko ya kinga njaa.

Alisema kampuni ya Ekari Moja Tanzania ni moja ya kampuni inayotoa pembejeo zenye uhakika ambazo zina ubora kuanzia kwenye mbegu na mbolea ni kitu ambacho wakulima wengi wamenufaika.

Alisema pia kampuni hiyo imekuwa msaada mkubwa kwa wakulima ikifundisha namna ya upandaji, palizi, uwekaji mbolea kwa awamu zote mbili ili mkulima kuzalisha mazao yenye ubora.

Ofisa kilimo katika kijiji cha Ivwanga, Angela Shoo, alisema wamekuwa wakishirikiana na Ekari Moja ambao wamekuja kwa ajili ya kusaidia kuongeza ufanisi wa kilimo kwa wakulima pamoja na wadau wengine wanaojishughulisha na masuala ya wakulima kwani serikali pekee isingeweza kuwafikia wakulima.

Ofisa mawasiliano wa kampuni ya Ekari Moja Tanzania, Dorcas Tinga, alisema kuwa kampuni hiyo inajishughulisha na ukopeshaji wa pembejeo kwa wakulima wadogo wadogo waliopo vijijini ambao hujiunga kwenye vikundi na kukopeshwa pembejeo.

Aliongeza kuwa wanatoa mafunzo kuanzia upandaji mpaka uvunaji ambapo mafunzo hayo hutolewa na maafisa shamba wa kampuni na kwamba matarajio yao kuhakikisha kuona kila kijiji kuwa na shamba darasa ambalo wakulima watakuwa wanajifunza masuala ya kilimo.

Alesi Mwantandi mkazi wa Mlowo, alisema kuwa kampuni ya Ekari Moja imekuwa msaada mkubwa kwa wakulima kwani kabla ya kupata elimu kutoka kampuni alikuwa akipata maunia 20, lakini kwa sasa anapata gunia 30 na kuendelea.





Baadhi ya wafanyabiashara wanaoanika dagaa katika eneo la Mangapwani wakiwa katika shughuli zao Mkoa wa Kaskazini Unguja.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# CUF yaomba Mashekhe Uamsho wasaidiwe fidia

**Na Rahma Suleiman**
ZANZIBAR

CHAMA cha Wananchi (CUF) Zanzibar, kimeiomba serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma viongozi wa Uamsho waliotoka gerezani kwa kuwalipa fidia ili kuanza harakati zao upya za maisha ya kila siku.

Hayo yalielezwa jana na Kaimu Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Mbarouk Seif Salum, wakati akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya chama hicho, Mtendeni Mjini Zanzibar.

Alisema kukaa kwao gerezani viongozi hao kumesababisha shughuli zao nyingi za kiuchumi kukwama na kupoteza vyanzo vyao walivyokuwa wakijitegemea kujiendesha kiuchumi.

"Kwa sasa tunaamini wapo taabani kiuchumi hivyo serikali kwa jicho lenye huruma liwaangalie mashekhe hao," alisema.

Kaimu Naibu Katibu Mkuu huyo, aliipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar kwa kuwaachia huru mashekhe hao.

Alitaka serikali kuendelea kuheshimu utawala wa sheria, haki za binadamu na demokrasia ikiwa ni miongoni mwa madaraja muhimu ya kufikia maendeleo endelevu katika taifa.

Aliiomba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuongeza nguvu kubwa ya kudhibiti mawasiliano ikiwamo ujumbe unaoleta uchochezi unaendelea kusambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii na yenye kufukua makaburi kuhusu kukamatwa kwa mashekhe hao jambo ambalo linaweza kuvuruga hali ya utulivu iliyopo.

Pia alivitaka vyama vya siasa vyenye lengo la kutumia fursa ya kutolewa gerezani kwa mashekhe hao kuwa ni ajenda yao ya kisiasa kufuta mara moja mawazo hayo. "Kufanya hivyo kunaweza kusababisha uchochezi mkubwa miongoni mwa wananchi na serikali yao...vyama vya siasa vifuate ajenda za msingi zenye lengo la kuwaunganisha wananchi, viongozi wao wa kidini pamoja na serikali yao," alisema.

Naibu huyo alisema pamoja na juhudi nyingine alizozichukua Rais Samia Suluhu Hassan, alimwomba kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa sheria kuwatoa gerezani wafungwa wote wa kisiasa ambao bado wanaendelea kusota katika magereza mbalimbali ili kwa pamoja kujenga Tanzania.

## 'Miundombinu kambi ya waanika dagaa hairidhishi'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Salum Mkuya, amefanya ziara katika kambi ya waanika dagaa iliyopo Mangapwani Mkoa wa Kaskazini Unguja na kushuhudia mazingira yasiyoridhisha kutokana na kukosekana kwa miundombinu muhimu.

Akizungumza katika eneo hilo, waziri huyo aliahidi kukaa na wahusika wa eneo hilo pamoja na kamati ya waanika dagaa ili kuondoa tatizo kwenye eneo hilo lenye harakati za kiuchumi kwa kuingia na kutoka wenyeji na wageni.

Hatua hizo ni pamoja na kupeleka wataalamu kutoka Mazingira, Tume ya Ukimwi na Tume ya Kitaifa Kuratibu na Kupambana na Dawa za Kulevya ili kutoa elimu kwa usalama wa waanika dagaa na wauzaji wa jumla kwenye kambi hiyo.

Alisema hatua nyingine ni pamoja na kuweka miundombinu ya uhakika ili kuepuka maradhi yanayoweza kutokea ikiwamo ya mlipuko kama kipindupindu.

Kwa upande wao wafanyabiashara wa eneo hilo, wamelalamikia kutofanyiwa kazi malalamiko yao ya muda mrefu ikiwamo kupatiwa huduma ya maji na vyoo na kushauri fedha zinazochangishwa na halmashauri kila mwezi kuwasaidia kuweka miundombinu ya kudumu.

Ali Juma, miongoni mwa wafanyabiashara wanaoanika dagaa katika eneo hilo, alisema kuwa kutokuwapo kwa huduma ya choo katika eneo hilo lenye mkusanyiko wa watu wengi kunahatarisha afya zao.

Aliiomba Serikali ya Zanzibar kuweka viwango maalum kwa wanunuzi wa dagaa kama inavyowekwa bei za mchele ili kuwakomboa kiuchumi.

Naye Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini, Mtumwa Peya, alikiri kuwa changamoto hiyo ni ya muda mrefu na tayari wameshakaa pamoja na kamati ya waanika dagaa kwa kushirikiana na sheha na kuziwasilisha changamoto hizo kwa Mkuu wa Wilaya Kaskazini 'B' Unguja.

Zaidi ya watu 400 waanika dagaa huweka kambi kwa wakati mmoja wakati wa msimu wa dagaa na wanunuzi wakubwa ni kutoka Kongo.

# Wilaya 33 kupatiwa chanjo ya kipindupindu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, inakusudia kutoa chanjo ya kudhibiti ugonjwa wa kipindupindu kwa wilaya 33, Unguja na Pemba.

Hayo yameelezwa na Mkurugenzi Kinga na Elimu ya Afya wa wizara hiyo, Dk. Fadhil Mohamed Abdalla, katika mafunzo ya waandishi wa habari ya uhamasishaji chanjo, Mnazimmoja mjini hapa.

Alisema, chanjo hiyo inayotarajiwa kufanyika kwa awamu kuanzia Julai 3-7, haina madhara kwa mwanadamu na inaingia katika mfumo wa chakula.

Alisema chanjo hiyo itawahusu wananchi wote isipokuwa watoto waliokuwa chini ya umri wa mwaka mmoja, watu wenye ujauzito na wagonjwa waliokuwapo chumba cha uangalizi (ICU).

"Chanjo hiyo inatarajia kufanyika kwa baadhi ya Wilaya za Unguja na Pemba, wito wetu ni wananchi wote kushiriki kwa zile wilaya zitakazohusika," alisema. Aliwataka wananchi kuendelea kuiunga mkono serikali kupitia Wizara ya Afya kwa kuwapa ushirikiano wataalamu watakaofika kutoa chanjo hiyo ili kuona maradhi hayo yanaondoka.

Alisema, chanjo hiyo imeshawahi kutolewa kwenye nchi za Msumbiji na Ethiopia na kuonesha mafanikio na kuwaondoa wananchi hofu kuhusu ubora wake.

"Chanjo hii imethibitishwa na Shirika la Kimataifa la Afya Duniani (WHO), na haina tatizo lolote kiafya," alisema.

Alisema, mwananchi atakayekamilisha chanjo hiyo kwa awamu mbili atakuwa na kinga kwa miaka mitatu na kusisitiza azma ya serikali ya kutokomeza maradhi hayo.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Afya kutoka Hospitali ya Mnazimmoja, Halima Ali Khamis, aliwataka wananchi kuendelea kufanya usafi katika maeneo yao na kunywa majisafi na salama na kunawa mikono kwa maji ya kutiririka ili kuendelea kujikinga na maradhi hayo.

Awali, chanjo hiyo iliwahi kutolewa mwaka 2009 na kuhusisha shehiya sita.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GODFREY BARAKA MPONZI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T. 266 BVR**, aina ya **SAN-LG M/CYLE**, yenye Chassis no. **LBRSP-JB55B9013162,** Engine no. **11940047.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi, **KAH/RB/TR/8500/2012.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MICHAEL ISRAEL LAISSER** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 926 CNE**. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: DSM/PHQ/RB/ **296944/2021.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na. 33 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**TUSWEGE IJANDE MWAIJANDE**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**DANFORD MWALUSAKO**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 20th Mwezi wa JULY, 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 16th Mwezi wa JUNE, 2021.

NAIBU MSAJILI

116318702

## VYETI VIMEPOTEA



**JOHARI JUMA NGWALE** anatangaza kupoteza vyeti vyake cha kumaliza kidato cha nne (4) chenye **Index No. S. 0264/0047** cha Shule ya Sekondari BARBRO JOHANSSON mwaka 2009. Cheti cha kumaliza kidato cha sita (6) chenye Index No. S0219/0514 cha Shule ya Sekondari ya Wasichana Songea mwaka 2012. vilivyotolewa na BARAZA LA MITIHANI TANZANIA (NECTA). Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **TUN/RB/1624/2021.**

116318402

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NO. 38/2019**
**(EXTENDED "J")**
**(Kutoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya,jinai No.68/2017)**
**JAMHURI…………………………MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**ELIAS KAYOWA……………………MJIBU RUFAA**
**KWA :**
**BWANA: ELIAS KAYOWA**
**POPOTE ULIPO -TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**

Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya Tarehe 24/06/2021 siku ya Jumatano saa 03.00 asubuhi bila kukosa.

ELEWA KWAMBA,ukikosa siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25/5/2021.

**Z.D.Laizer**
**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**
**MBEYA**

26316802

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na. 55 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU ROMAN SADI MOSHI**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**PRISCA ROMAN MOSHI & PROCHES ROMAN MOSHI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30th Mwezi wa JUNE, 2021.

Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe……Mwezi wa……..2021.

NAIBU MSAJILI

116318602

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie**
**0782253676**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Marekani yahofia wimbi ugaidi Afrika

**Rabat,** MOROCCO

MKUU wa Kikosi cha Marekani kwa ajili ya Afrika, Jenerali Stephe Townsend, ameonya wimbi la ugaidi linalolikumba bara la Afrika hivi sasa, akisema linabidi kushughulikiwa na dunia nzima.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa zoezi kubwa la pamoja la kijeshi kati ya wanajeshi wa Marekani, Afrika na Ulaya linalofahamika kama African Lion, mkuu wa Africom alipongeza kazi iliyofanyika wiki mbili za mazoezi pia kutoa taswira ya vitisho vionavyojitokeza katika sehemu kadhaa za Afrika.

Jenerali Townsend aliwaambia waandishi wa habari mjini Rabat ambako mazoezi yalimalizikia kwamba ana wasiwasi kutokana na hali ya usalama katika pembe mbalimbali za bara hilo kuanzia Kanda ya Sahel upande wa Magharibi hadi Pembe ya Afrika.

Alisema mashambulio ya hatari yanayofanywa na makundi yenye uhusiano na Al-Qaida na Islamic State pamoja na wanamgambo wa al-Shabaab yanaendelea kuongezeka.

Anasema mataifa jirani ya Afrika, yanasaidia serikali zinazokabiliwa na vitisho hivyo na kwamba juhudi zote zinaonekana hazitoshi kusitisha kile anachokieleza ni moto wa msituni wa ugaidi unaokumba bara hilo.

Zoezi la African Lion liliwahusisha wanajeshi elfu saba, kutoka nchi saba pamoja na ushiriki wa NATO kwa kufanya mazoezi ya anga nchi kavu na bahari kwa pamoja huko Moroco, Tunisia na Senegal.

**VOA**



Mtoto akiwa katika kambi ya wakimbizi eneo la Peshawar, Pakistan. Juni 20, ni Siku ya Wakimbizi Duniani, huku nchi hiyo ikiwa na takribani wakimbizi milioni 1.5 kutoka nchi mbalimbali. Zaidi ya watu milioni 82.4 duniani hawana makazi, kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR). **PICHA: EPA**

## Iran huenda ikarejea msimamo mkali

**Tehran,** IRAN

IRAN inatarajiwa kuhamia kwenye msimamo mkali zaidi dhidi ya mataifa ya Magharibi chini ya Ebrahim Raisi, mwanazuoni mhafidhina wa sheria ya Kiislam na Jaji Mkuu, ambaye ameshinda uchaguzi wa urais humo.

Rais alipata ushindi wa kishindo kwa asilimia takribani 62 ya kura zote zilizopigwa Ijumaa, mwishoni mwa wiki.

Anatarajiwa kuingia mamlakani mwezi Agosti, mwaka huu.

Rais anatarajiwa kuingiza utawala wa kihafidhina wa kuipinga Marekani katika kipindi cha miaka minane, akibadili mwelekeo kutoka kwa sera za Rais wa sasa Hassan Rouhani za kutafuta mazungumzo na nchi za Magharibi.

Juzi, Rais alielezea nia yake ya kufanya kwa ubora ili kutimiza majukumu yake kwa ajili ya watu wa Iran, baada ya kuzungumza na rais anayeondoka madarakani Jumamosi, wiki ijayo.

Rais ameashiria kuwa ataendelea kudumisha makubaliano ya nyuklia na mataifa yenye nguvu duniani. Rais wa zamani wa Marekani Donald Trump aliamua kuiondoa nchi yake katika makubaliano hayo mwaka 2018.

Marekani na Iran zimekuwa zikifanya majadiliano yasiyokuwa ya moja kwa moja, yaliyolenga katika kufufua makubaliano ya nyuklia tangu mwezi Aprili.

Hata hivyo, Rais ameapa kutofanya makubaliano yoyote kirahisi.

Zaidi ya waungaji mkono 1,000 wa Rais walishangilia ushindi wake kwa fataki jijini Tehran. Walikuwa wakishika picha za Rais na kutaja jina lake. **NHK**

## Brazil vifo 500,000 vya Covid-19

**Rio de Jeneiro,** BRAZIL

BRAZIL imekuwa taifa la pili duniani baada ya Marekani, ambayo idadi yake ya vifo kutokana na janga la COVID-19, imepitiliza 500,000.

Ongezeko hilo la idadi ya vifo katika taifa hilo la Kusini mwa Amerika, linajiri wakati nchi hiyo inakumbwa na wimbi la tatu la maambukizi ya virusi vya corona.

Wizara ya Afya iliripoti jumla ya vifo 500,800 ikiwa ni pamoja na watu 2,301 waliofariki ndani ya saa 24 zilizopita.

Hayo yakijiri, maelfu ya waandamanaji walijitokeza katika mji wa Rio de Janeiro na miji mingine kadhaa kulalamika kuhusu namna rais wa nchi hiyo, Jair Bolsonaro anavyolishughulikia janga la virusi vya corona.

Wamemshtumu kwa kutonunua chanjo za virusi hivyo kwa haraka na pia ukaidi wake dhidi ya kuvaa barakoa. **DW**

## Japan kuondoa hali ya dharura mikoa 8

**Tokyo,** JAPAN

SERIKALI ya Japan imemaliza hali ya dharura ya virusi vya corona jijini Tokyo na mikoa mingine minane, jana.

Ni mkoa wa Okinawa pekee, ambao utabaki katika hali ya dharura hadi Julai 11, mwaka huu.

Mikoa saba kati ya minane ikiwa ni pamoja na Tokyo na Osaka hali ya dharura itabadilishwa kwa hatua madhubuti ambazo zitaanza kutekelezwa kesho Jumatatu.

Katika maeneo hayo ambako hatua madhubuti zitatekelezwa, migahawa na vilabu vya pombe ambavyo vitakidhi vigezo fulani vitaruhusiwa kuhudumia kilevi hadi saa moja jioni.

Jijini Tokyo, kilevi kinaweza kuhudumiwa kwa wateja ambao wapo peke yao ama katika kikundi cha watu wawili ambao hawakai zaidi ya dakika 90.

Serikali imedhamiria kufanya kazi kwa karibu na mikoa ili kuhakikisha kuwa sheria zinafuatwa, ambapo virusi vimekuwa vikionekana kusambaa mahali ambapo vyakula na vinywaji vinahudumiwa.

Juzi, Waziri Mkuu Suga Yoshihide alibadilishana maoni juu ya mlipuko huo jijini Tokyo na Gavana Koike Yuriko wa jiji hilo. **NHK**

## Guinea yatangaza kuimaliza ebola

**Conakry,** GHANA

GUINEA imetangaza kumaliza mlipuko wa hivi karibuni wa ebola kwenye taifa hilo la Afrika Magharibi, ikiwa ni karibu miezi minne baada ya virusi vya ugonjwa huo kuanza kuenea nchini humo.

Waziri wa Afya Remy Lamah, alitangaza hatua hiyo kwenye mkutano na waandishi wa habari juzi, Shirika la Afya Duniani-WHO limesema limethibitisha maambukizi 23, yakiwamo yale yanayodhaniwa kuwa ni ugonjwa huo na vifo 12.

WHO ilianza kushirikiana na serikali ya Guinea kuanzia hatua za mwanzoni za mlipuko wa ugonjwa huo.

Shirika hilo lilisaidia kutoa chanjo kwa watu takribani 10,000 na kutuma wataalamu kutoa msaada wa matibabu. **NHK**

# MONACO YAJITOSA KWA BOATENG




**MONACO,** Ufaransa

KLABU ya As Monaco imeanza mazungumzo na wawakilishi wa mlinzi wa zamani wa Bayern Munich, Jerome Boateng ili kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto.

Kocha Mkuu wa Monaco, Niko Kovac, amewaambia viongozi wa klabu hiyo anamhitaji mlinzi huyo ili kupata mtu mzoefu katika idara hiyo.

Mbali na uongozi wa AS Monaco kuwa katika mpango wa kumsajili mlinzi huyo, lakini wanakabiliwa na upinzani kutoka AS Roma na Lazio ambao wote wameonyesha dhamira ya kutaka kumsajili mlinzi huyo majira haya.

Boateng alitangaza kuachana na Bayern Munich baada ya kushindwa kufikia makubaliano na miamba hao wa Ujerumani juu ya mkataba mpya aliohitaji kuongeza klabuni hapo.

Boateng mchezaji wa zamani wa timu ya Taifa ya Ujerumani mwenye asili ya Ghana, alikataa ofa aliyopewa na Munich na hivyo kuamua kuondoka kama mchezaji huru, ambapo mkataba wake unamalizika Juni 30, mwaka huu.

# Ancelotti kukomba nyota wa Everton

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti anaangalia uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin ili kutua pale Santiago Bernabeu, kwa mujibu wa The Sun.

Real Madrid ni moja ya klabu ambayo kwa sasa ipo bize sokoni kutafuta wachezaji wapya kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake.


Ancelotti aliteuliwa kuchukua mikoba ya kuinoa Madrid kwa mara ya pili mapema mwezi uliopita akitokea kule Everton.

Na sasa Ancelotti ambaye ni raia wa Italia, anakijenga upya kikosi hicho na jicho lake limetua kwa Calvert-Lewin ambaye alikuwa na wakati mzuri zaidi kule Everton wakati yeye akiwa kocha.

Kwa mujibu wa ripoti, Madrid wapo tayari kutoa ofa ya pauni milioni 50 ili kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa England.

Pamoja na straika huyo, Ancelotti pia anataka kumchukua James Rodriguez kutoka kule Goodison Park, ambaye awali alikuwa Madrid kabla ya kwenda Everton.

Pia mkali wa Sevilla, Jules Kounde yupo kwenye rada za Ancelotti ambapo ada yake inatajwa kuwa ni Euro milioni 80.






# *Tierney kupewa mitano Arsenal*

**LONDON,** England

NYOTA Kieran Tierney ameripotiwa kufikia hatua kubwa ya mazungumzo na klabu yake ya Arsenal juu ya mkataba mpya wa miaka mitano.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amecheza mechi 62 na 'Washikabunduki' hao tangu alipowasili hapo akitokea Celtic mwaka 2019 na bado amebakiza miaka mitatu kutekeleza mkataba wake wa sasa kwenye Uwanja wa Emirates.

Tierney alifanikiwa kwa kiasi fulani chini ya Mikel Arteta wakati wa kampeni ya 2020-21, akichangia mabao mawili na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 38 kwenye mashindano yote.

Kwa mujibu wa Telegraph, Arsenal imefikia hatua kubwa ya kukamilisha mazungumzo na mchezaji huyo wa kimataifa wa Scotland kuhusu mkataba mpya wa miaka mitano, ambao utaonyesha umuhimu wake kwa timu hiyo.

Ripoti zinadai kwamba klabu hiyo ya London Kaskazini, ambayo pia inasemekana kuwa katika mazungumzo na Ben White wa Brighton & Hove Albion, wana matumaini ya kumaliza mazungumzo katika siku zijazo.

## HABARI MICHEZO

# Giroud afikisha mechi 100 chini ya Deschamps

**PARIS,** Ufaransa

OLIVIER Giroud ameweka historia ya kufikisha mechi 100 kuichezea Ufaransa chini ya kocha Didier Deschamps.

Hakuna mchezaji mwingine wa 'Les Bleus' hao ambaye amefikisha idadi kama hiyo ya mechi za timu ya wakubwa chini ya kocha huyo.

Straika huyo wa Chelsea, ambaye alianza kuichezea Ufaransa Novemba mwaka 2011, alicheza mechi zake nane za mwanzo chini ya Laurent Blanc, ambaye alijiuzulu baada ya Euro 2012.

Deschamps alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo Julai 2012 na tangu hapo amemfanya Giroud kuwa kwenye mipango yake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alicheza mechi yake ya 100 chini ya kiungo huyo wa zamani Jumamosi wakati Ufaransa ikitoka sare ya bao 1-1 na Hungary kwenye Euro 2020, Jumamosi.

Wachezaji wengine waliocheza mechi nyingi kumkaribia Giroud chini ya Deschamps ni Antoine Griezmann (mechi 93), Hugo Lloris (90), Paul Pogba (82) na Blaise Matuidi (80).

Giroud amefunga mabao 45 katika mechi zake 99 chini ya Deschamps, yakiwamo 16 kwenye mashindano ya Ulaya.

Alifunga bao moja tu kwenye mechi 12 za Kombe la Dunia, ingawa alicheza kila mchezo wakati Ufaransa ikitwaa ubingwa huo mwaka 2018 nchini Urusi.

Bao la kwanza la Giroud chini ya Deschamps, alifunga dhidi ya Hispania wakati wa kufuzu Kombe la Dunia Oktoba mwaka 2012, huku pia akifunga 'hat-trick' kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Paraguay, Juni 2017.





# DE BRUYNE: NIKO FITI SIHOFII MAJERAHA

**BRUSSELS,** Ubelgiji

KEVIN De Bruyne hana hofu na hali yake kiafya baada ya kuichezea Ubelgiji mechi yake ya kwanza kwenye michuano ya Euro 2020 akitoka kujiuguza.

Nyota huyo wa Manchester City aliumia pua baada ya kugongana na mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger kwenye mchezo wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baina ya timu hizo, mwezi uliopita.

Hata hivyo, kuumia huko hakukumfanya kuachwa kwenye kikosi cha Ubelgiji chini ya kocha Roberto Martinez, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, hakuweza kucheza mchezo wa kwanza kwenye mashindano hayo ya Euro 2020.

Baada ya kuukosa mchezo huo wa kwanza wa Ubelgiji kwenye Kundi B ambao walishinda mabao 3-0 dhidi ya Urusi, De Bruyne alitokea benchi kwenye mchezo wa ushindi wa 2-1 dhidi ya Denmark, na yeye akifunga la ushindi.

Na sasa Ubelgiji imepaa kileleni mwa msimamo wa Kundi B na itacheza na Finland pale Saint Petersburg leo, Jumatatu na De Bruyne na amesema amejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo huo na hana hofu na majeraha yake.

# *Hispania itafuzu 16-bora Euro - Alba*

**SEVILLE,** Hispania

JORDI Alba anahisi Hispania ilistahili kuifunga Poland na amebaki akijiamini kwamba, watafuzu kwenye hatua ya raundi ya 16 baada ya sare ya 1-1 kwenye michuano ya Euro 2020 katika Uwanja wa La Cartuja, Juzi.

Alvaro Morata aliwaweka mbele La Roja hao kipindi cha kwanza na kumaliza ukame wa mechi nne za kimataifa bila bao, akinyamazisha pia shutuma alizopewa baada ya kushindwa kufunga dhidi ya Sweden.

Hispania walishindwa kupata ushindi wao wa kwanza wa michuano hiyo, baada ya Robert Lewandowski kusawazisha kipindi cha pili kwa kichwa na kuiweka Poland kuwa na matumaini ya kusonga mbele.

Hispania inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo na watacheza na Slovakia Jumatano kwenye mchezo wa mwisho wa kundi hilo la E na Alba amesema ana uhakika watafuzu kwa hatua inayofuata ya michuano hiyo.

"Ninaamini tutasonga mbele kwenye hatua inayofuata, tutapata ushindi katika mchezo wetu unaofuata," alisema mlinzi huyo wa kushoto wa Barcelona.

"Nafikiri hakuna shaka ya kuhofia, ninaimani kubwa kwamba tutaweza kufuzu bila tatizo lolote, kwani kikosi tulicho nacho kinaweza kufanya hivyo."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# BARCELONA YATHIBITISHA RASMI KUMSAJILI DEPAY

Akimaliza majukumu yake na timu ya taifa kwenye Euro 2020, ataelekea moja kwa moja...

**BARCELONA,** Hispania

MEMPHIS Depay amethibitishwa kuwa ni mchezaji wa Barcelona, huku nyota huyo wa Uholanzi akijiunga na timu hiyo kwa uhamisho huru kutoka Lyon ya Ufaransa.

**Depay kwa sasa yupo na kikosi cha Uholanzi kwenye michuano ya Euro 2020, huku penalti yake dhidi ya Austria Alhamisi ilikisaidia kikosi hicho cha kocha Frank de Boer kufuzu hatua ya mtoano kwenye Euro 2020 kutoka Kundi B, baada ya ushindi wa mabao 2-0.**

Depay akimaliza majukumu yake na timu ya taifa, atajiunga rasmi na Barcelona ambayo imekuwa ikitajwa kumwania kwa muda mrefu nyota huyo wa zamani wa Manchester United.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye alijiunga na Lyon msimu wa 2016-17 baada ya kushindwa kung'ara kule Old Trafford, atasaini mkataba wa miaka miwili na Barca mara tu mkataba wake wa sasa na miamba hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, utakapomalizika Juni 30.

Depay alikuwa na wakati mzuri zaidi pale Lyon na kule Barca anakwenda kujiunga na kocha wake wa zamani wa timu ya Taifa ya Uholanzi, Ronald Koeman.

Msimu wake wa mwisho pale Lyon alifunga mabao 20 kwenye Ligue 1, akishika nafasi ya pili nyuma ya mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe (mabao 27), huku akiwa na pasi za mwisho 12 na alitengeneza nafasi 94.

Depay anakuwa mchezaji wa nne kusajiliwa pale Barcelona msimu huu, baada ya ujio wa Sergio Aguero, Eric Garcia - wote wakijiunga kwa uhamisho huru kutoka Manchester City na mlinzi wa kulia Emerson.

Hata hivyo, walishindwa kumsajili mchezaji mwenzake na Depay kwenye kikosi cha Uholanzi, Georginio Wijnaldum, ambaye aliamua kujiunga na PSG baada ya mkataba wake na Liverpool kumalizika.

## ZISIKUPITE

### PAUNI MIL 100 KWA KANE

MANCHESTER City italazimika kutoa dau la pauni milioni 100 ili kumnunua mshambuliaji wa England Harry Kane 27. ***(Star)***

### UNITED YARUDI KWA SANCHO

MANCHESTER United imewasilisha ombi jipya kwa mchezaji wa Borrusia Dortmund na England mwenye thamani ya pauni milioni 75, Jadon Sancho, 21, baada ya ofa ya awali ya pauni milioni 67 kukataliwa na klabu hiyo ya Ujerumani. ***(Mail)***

### TRIPPIER AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Paris St-Germain imejiunga na Manchester United katika mbio za kuwania kumsajili beki wa England, Kieran Trippier, 30, kutoka Atletico Madrid. ***(France Football via Mundo Deportivo)***

### RODRIGUEZ KURUDI MADRID

USAJILI mkubwa wa Real Madrid msimu huu unaweza kuwa ule wa kurudi kwa winga wa Colombia, James Rodriguez, 29, kutoka Everton. ***(Sport)***

### TIERNEY MIAKA MITANO

MLINZI wa kushoto wa Scotland, Kieran Tierney, 24, ataongeza mkataba wa miaka mitano na Arsenal. ***(Guardian)***

### LOFTUS-CHEEK KUUZWA

CHELSEA iko tayari kumuuza kiungo wa kati, Ruben Loftus-Cheek mwenye umri wa miaka 25, kwa klabu ya Inter Milan ikiwa ni sehemu ya mpango wa kumtwaa Achraf Hakimi, 22. ***(Gazzetta dello Sport)***

### EDOUARD KUTUA WEST HAM

WEST Ham inafikiria kumsajili mshambuliaji wa Celtic, Odsonne Edouard, 23. ***(Mail)***

### DAKA ATUA LEICESTER

LEICESTER City imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa klabu ya Red Bull Salzburg, Patson Daka, 22, raia wa Zambia. ***(Football Insider)***

### PATRICIO KUJIUNGA NA ROMA

GOLIKIPA wa Ureno na Wolves, Rui Patricio, 33, amefikia makubaliano ya kujiunga na klabu ya AS Roma. ***(Sky Sport)***

### MADRID KUMUUZA JOVIC

REAL Madrid inafirikia kumuuza Luka Jovic, 23, huku klabu yake ya zamani Eintracht Frankfurt ikiwa na nia ya kumsajili upya mshambuliaji huyo wa Serbia. ***(AS)***

### LIVER YAMSAJILI ISSAHAKU

LIVERPOOL imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa Ghana, Abdul Fatawu Issahaku mwenye umri wa miaka 17, kwa mujibu wa klabu ya Steadfast FC. ***(Mirror)***

## HABARI MICHEZO

# KMC vs Mtibwa, Namungo, Azam vitani leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha wakusanya ushuru wa Kinondoni (KMC FC), leo kitashuka dimbani kuivaa Mtibwa Sugar kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania, utakaopigwa Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam huku Namungo FC ikiikaribisha Azam FC kwenye Dimba la Majaliwa mkoani Lindi.

KCM FC itaikaribisha Mtibwa Sugar ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza kwa bao 1-0 kwenye mchezo wa mzunguko wa kwanza uliopigwa mjini Morogoro.

Hata hivyo, timu hizo zitakutana KMC ikiwa nafasi ya saba baada ya kushuka dimbani mara 30 na kujikusanyia pointi 41 huku Mtibwa Sugar yenyewe ikiwa na nafasi ya 11 na alama zake 37 zilitokana na michezo 31.

Lakini KMC FC wanashuka dimbani wakitoka kupoteza 1-0 kwenye mechi iliyopita dhidi ya Dodoma Jiji FC, uliopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na Mtibwa Sugar nao wakitoka kushinda bao 3-1 dhidi ya Mwadui FC katika Uwanja wa Kambarage, Shinyanga.

Wakizungumza na gazeti hili jijini jana Makao Makuu ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Kocha Mkuu wa KMC FC, Habib Kondo, alisema mechi hiyo kwao itakuwa ngumu kwa sababu wanakutana na timu ambayo iko katika nafasi ya kujinasua kushuka daraja.

"Hatuangalii mechi iliyopita hiyo ilikuwa maandalizi ya mechi yetu ijayo dhidi ya Mtibwa Sugar, timu nzuri na wanahitaji kupata matokeo mazuri, kujiweka katika nafasi nzuri ya kuendelea kusalia katika ligi hiyo," alisema Kondo.

Naye Kocha wa Mtibwa Sugar, Mohammed Badru, alisema vijana wake wako fiti na kila mechi kwao ni fainali ili kupata pointi muhimu kujiweka katika nafasi nzuri ya kujinasua kubaki katika ligi hiyo.



Kikosi cha Taifa Stars kilichoanza dhidi ya Malawi na kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# SBL YAKUNWA KIWANGO TAIFA STARS BILA MASTAA

**Na Mwandishi Wetu**

MDHAMINI mkuu wa timu ya Taifa, Taifa Stars, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia Bia ya Serengeti Lager, imeeleza kuridhishwa na kiwango cha timu hiyo baada ya ushindi mzuri wa mabao 2-0 iliyoupata hivi karibuni dhidi ya timu ya Taifa ya Malawi.

**Siku chache kabla ya mechi hiyo ya kirafiki iliyochezwa Juni 13, mwaka huu Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, SBL ilileza kuridhishwa na kikosi kilichotangazwa na kocha wa timu hiyo, Kim Paulsen na kuitabiria ushindi jambo ambalo lilitimia.**

Pamoja na kutokuwa na wachezaji wake wa kimataifa na inaowategemea wakiwamo Mbwana Samatta na Simon Msuva, Taifa Stars ilionyesha kandanda safi katika mechi hiyo ya kimataifa ambayo ipo katika Kalenda ya FIFA na kuilaza Malawi kwa mabao 2-0.

Taifa Stars ikiongozwa na nahodha wake, John Bocco iliutawala mchezo na kuwafurahisha Watanzania Pamoja na wapenzi wa soko baada ya kumaliza dakika 90 wakiondoka kifua mbele.

Akizungumzia ushindi huo Mkuu wa Kitengo cha bia ya Serengeti Lager, Wankyo Marando, aliipongeza Taifa Stars pamoja na benchi zima la ufundi kwa matokeo mazuri.

"Tukiwa kama wadhamini wa Taifa Stars, tunafurahishwa sana na matokeo mazuri dhidi ya Malawi. Tunaamini huu ni mwanzo tu wa ushindi wa kishindo ambao Taifa Stars itaendelea nao katika kila mechi yake," alisema.

Wankyo alisema SBL kupitia bia yake ya Serengeti Lager, itaendelea kuwa shabiki namba moja wa Taifa Stars na kwa kuiunga mkono timu hiyo ili kufanya vizuri katika mechi zake.

"Chapa ya Serengeti ni mdau mkubwa wa michezo hapa nchini na tunaona furaha kuchangia maendeleo ya michezo na tunaahidi kuendelea kuhamasisha na kuchangia maendeleo ya sekta hii ambayo pia huwaleta watu pamoja," alieleza.

Mwaka jana, Bia ya Serengeti Premium Lager iliingia mkataba wa miaka mitatu na TFF na kuwa mdhamini mkuu wa Taifa Stars kwa makubaliano ya kutoa kiasi cha shilingi bilioni tatu katika kipindi cha mkataba huo. Mkataba huo umekuja baada ya kumalizika ule wa awali ambao pia ulikuwa ni wa miaka mitatu uliosainiwa mwaka 2017.

## KI-4G...



Msanii wa kizazi kipya kutoka Kundi la Wasafi, Zuhura Othman Soud maarufu Zuchu akitumbuiza wakati wa tamasha la Pasua Anga Ki Zantel 4G, lililofanyika Jumamosi katika viwanja vya Kisonge, Unguja. Msanii huyo ni balozi wa Zantel 4G ikiwa ni mpango wa kuelimisha wateja juu ya matumizi sahihi ya mtandao wa 4G kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Mtibwa mabingwa U-20*

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

TIMU ya Mtibwa Sugar chini ya miaka 20, imefanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi ya Vijana Tanzania Bara chini ya miaka hiyo, kwa kuichapa Yanga mabao 2-1 kwenye mechi kali ya fainali iliyochezwa juzi usiku katika Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Walikuwa Omari Marungu aliyefunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 10 na Richard Mwamba dakika ya 24, waliyoifanya Mtibwa kuwa mbele kwa mabao 2-0 hadi mapumziko.

Kipindi cha pili vijana wa Yanga walibadilika na kuja juu, kiasi cha kufanikiwa kupata bao la kufutia machozi dakika ya 82, likifungwa na mchezaji wao tegemeo, Abdulkarim Yunus.

Ni mchezaji huyo huyo aliyeukwamisha tena mpira wavuni dakika ya 88, lakini kabla ya hapo tayari mwamuzi wa pembeni alikuwa amenyoosha kibendera.

Baada ya hapo baadhi ya mashabiki wa Yanga waliokuwa uwanjani hapo, walifanya vurugu na kusababisha mpira kusimama.

Huo unakuwa ni ubingwa mara ya tatu mfululizo kwa timu hiyo, huku ikitoa kiungo bora wa michuano hiyo ambaye ni Joseph Mkele na mfungaji bora Omari Marundu aliyepachika mabao sita.

Pia kocha wa Mtibwa Sugar, Awadh Juma, amechaguliwa kuwa kocha bora wa michuano hiyo.

Kipa wa Yanga, Geofrey Magaigwa, amechaguliwa kuwa kipa bora, huku Ally Mohamed Said wa klabu hiyo akichaguliwa kuwa beki bora.

Michezo
Jumatatu Juni 21, 2021
Nipashe



Barca yathibitisha kumsajili Depay UKURASA 22

CHA 3 HICHO...




Kiungo mshambuliaji wa Ujerumani, Kai Havertz, akiifungia timu yake bao la tatu katika ushindi wa mabao 4-2 walioupata dhidi ya Ureno kwenye mechi ya michuano ya Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Allianz Arena jijini Munich, Ujerumani juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Simba: Sasa vumbi la pointi tu, mabao basi

## ●●● Yasema hata dozi ya moja moja inatosha, yaacha mbio ndefu kwa Yanga, Azam...

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kuambulia ushindi wa bao 1-0 kwa tabu dhidi ya Polisi Tanzania juzi, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, amesema walichokuwa wanakihitaji ni pointi tatu tu na si idadi kubwa tena ya mabao kwa kuwa kwa upande huo wana mtaji wa kutosha.

**Simba ipo kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 70 na mabao 65 ya kufunga na 11 ya kufungwa baada ya kushuka dimbani mara 28, huku Yanga inayoshika nafasi ya pili ikiwa na alama 64 na mabao 46 ya kufunga na 19 ya kufungwa, yaliyotokana na michezo 30.**

Azam inafuata katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 63 na mabao 48 yakufunga na 21 ya kufungwa baada ya kushuka dimbani mara 31 kwenye ligi hiyo inayojumuisha timu 18 msimu huu.

Akizungumza baada ya mechi hiyo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, Simba ikipata ushindi huo kupitia faulo iliyopigwa na Luis Miquissone, Matola alisema haiwezekani kila mechi timu icheze kama inavyokuwa siku zote na hasa ukichukulia kuwa wachezaji wengi wametoka kwenye mapumziko ya mechi za Kalenda ya FIFA za timu za taifa.

"Tumepata pointi tatu. Hicho ndicho kikubwa. Kama nilivyosema mwanzo kabla ya mechi kuwa hautokuwa mchezo rahisi, hasa sisi tukikutana na Polisi Tanzania, huwa mechi ngumu, japo mechi zote nne tulizocheza nao tumeshinda. Tunashukuru kwa tulichokipata kwa sababu haiwezekani timu ikacheza vizuri kila siku," alisema Matola.

Alisema kwa jinsi hali ilivyofikia, Simba inahitaji zaidi pointi tatu kuliko mabao kwani inayo ya kutosha. Kwenye mechi hiyo, Simba haikuwa kwenye kiwango bora kama ilivyozoeleka.

Naye Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alisema aliwaambia wachezaji wake waepuke sana kucheza faulo karibu na maeneo ya hatari, lakini hawakumsikiliza na matokeo yake hata bao la Simba lilitokana na mpira wa adhabu.

Alisema kwenye mechi hiyo walicheza vema, lakini tatizo lao lilikuwa ni kuweka mpira ndani ya wavu na huenda ilitokana na kutojiamini kwa wachezaji wake, kwani walikuwa wanacheza na timu kubwa ya Simba.

"Kuna nafasi mchezaji wangu alipata akiwa na Aishi Manula, lakini akapoteza. Pia niliwaambia wachezaji wangu wasifanye faulo za mara kwa mara kwenye eneo la hatari, na kweli ndiyo iliyozaa bao, lakini pamoja na hayo wachezaji wangu wamepambana sana," alisema Malale ambaye matokeo hayo yanaifanya timu yake ibaki nafasi ya nane ikiwa na pointi 41 baada ya michezo 31.

Simba itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho kuikaribisha Mbeya City kwenye ligi hiyo wakati Polisi Tanzania ikisubiri hadi Alhamisi wiki hii kuifuata Ruvu Shooting.

## Rekodi 5 za kuvunjwa na Ronaldo Euro 2020

**LISBON,** Ureno

JINA la Cristiano Ronaldo limejaa rekodi ya kila aina kwenye soka na sasa linatajwa...



HABARI UK. 11

## KMC FC vs Mtibwa, Namungo, Azam leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha wakusanya ushuru wa Kinondoni (KMC FC), leo kitashuka dimbani...



HABARI UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >